
**Bunge** lawaweka matatani vigogo wa halmashauri
UKURASA 4



**Daktari** bingwa watoto afariki, wengi wamlilia
UKURASA 4



UKURASA 11

Jumamosi Agosti 14, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe
MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580672
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Sabaya awataja JPM na Mpango

**ORODHA** yamgusa pia Gavana wa BoT... *Endelea ukurasa 3*



Hayati Rais Dk. John Magufuli



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango



Gavana Prof. Florens Luoga



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Rais na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Elsewedy Electric ya nchini Misri, Mhandisi Ahmed El Sewedy, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Rais Samia, mwekezaji wateta fursa ajira, uchumi
UKURASA 2

UKURASA WA 7

## WALIA UENDESHAJI MWENDOKASI, KUJAZWA ABIRIA

BAADHI ya abiria wanaotumia magari ya Chake Chake-Muambe na Mkoani-Muambe mkoa wa Kusini Pemba wamelalamikia madereva kwa kuendesha mwendo kasi na kupakia kupita kiasi. Wamesema jambo hilo linawakwaza na hata...

UKURASA WA 8

## MRUNDIKANO WANAFUNZI KIBAHA KUWA HISTORIA

TATIZO la mrundikano wa wanafunzi katika Shule ya Msingi Mtongani, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, liko mbioni kumalizika baada ya kukamilika kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa na ofisi ya...

UKURASA WA 9

## VIJANA WAONYWA TAMAA MAISHA YA MKATO

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi, amewataka vijana kufanya kazi na kuacha tamaa ya kuwa na maisha mazuri kwa muda mfupi. Katambi aliyasema hayo jana alipozungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Vijana Kimataifa..

# Kesi ya Mbowe yachukua sura mpya
UKURASA 2

**MICHEZO** **CHAMA, KISINDA SASA TIMU MOJA** UK. 24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Rais Samia, mwekezaji wateta fursa ajira

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS Samia Suluhu Hassan amekutana na kufanya mazungumzo na Rais na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Elsewedy Electric kutoka Misri, Ahmed El Sewedy, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma.

Katika mazungumzo hayo yaliyofanyika jana, El Sewedy alimfahamisha Rais Samia kuwa kampuni yake mbali na kuwa miongoni mwa kampuni zinazojenga mradi wa kuzalisha umeme katika Bwala la Mwalimu Nyerere, pia imewekeza katika miradi mingine na kutarajia kuwekeza zaidi nchini.

El Sewedy alisema kampuni yake inajenga mitambo ya kuzalisha umeme wa megawati 2115 katika Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Pia alisema katika eneo la Kigamboni jijini Dar es Salaam, kampuni yake imejenga kiwanda cha kuzalisha nyaya za umeme, transfoma, vifaa vya kuzuia nyaya za umeme zisilete hitilafu na mita za umeme, ambacho kinatarajiwa kufunguliwa rasmi Desemba, mwaka huu.

Alisema kutokana na mazingira mazuri ya uwekezaji yanayoendelea kuwekwa na serikali, wameamua kuunga mkono na kuwekeza zaidi kwa kujenga eneo la viwanda lenye ukubwa wa mita za mraba milioni mbili ikiwamo ujenzi wa kiwanda cha mbolea.

El Sewedy aliongeza kuwa anatarajia kuwekeza katika ujenzi wa reli ya kisasa na katika kipindi cha miaka miwili, atahamasisha kampuni takriban hamsini kutoka Misri kuja kuwekeza nchini.

Rais Samia alimshukuru El Sewedy na kumhakikishia serikali itampa ushirikiano katika kutekeleza miradi hiyo ya maendeleo kwa muda mwafaka.

Mkuu wa nchi huyo alisema ujenzi wa eneo maalum la viwanda litasaidia kuchangia kwa kiasi kikubwa utoaji wa ajira na ujuzi.

Rais Samia alimjulisha mwekezaji huyo kuwa kwa sasa Tanzania inapitia sheria na sera zake mbalimbali ili kujenga mazingira mazuri zaidi ya biashara na uwekezaji.



Wakili Peter Kibatala akizungumza na waandishi wa habari nje ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kesi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kesi inayomkabili Mbowe yachukua sura mpya

**Na Kulwa Mzee**

KESI ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu, imechukua sura mpya baada ya washtakiwa kuwasilisha notisi wakiomba mahakama ipeleke Mahakama Kuu matamshi yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu kwa madai yanaathiri kesi.

Hoja hizo ziliwasilishwa na Wakili Peter Kibatala, jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, kwenye Ukumbi wa Mahakama Mtandao wakati kesi hiyo ilipotajwa humo kwa sababu washtakiwa hawakupelekwa mahakamani.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, alidai wakati kesi inatajwa, washtakiwa walioko Gereza la Ukonga ni watatu; Halfani Hassan, Mohammed Lingwenya na Mbowe na mwingine Adam Kasekwa yuko Gereza la Segerea na wote hawakupelekwa mahakamani kwa sababu ya tatizo la usafiri.

Wakili Hillar aliomba shauri liendelee Gereza la Ukonga kisha mahakama ihamie Segerea kwa ajili ya mshtakiwa aliyekuwa huko. Mahakama ilifanya hivyo.

Wakili huyo pia alidai taarifa iliyotakiwa kuwasilishwa ili kukamilisha utaratibu kwa washtakiwa kusomewa maelezo ya mashahidi na kesi ihamie Mahakama Kuu, haijawa tayari.

Akijibu hoja za Upande wa Jamhuri, Wakili Kibatala alidai kesi ilikuwa inakuja kwa ajili ya kusikilizwa na Agosti 12, mwaka huu walwasilisha notisi chini ya kifungu namba 9(1) cha Sheria ya Haki za Binadamu Sura ya 3 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, wakidai kutokana na matamshi yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Samia Suluhu Hassan, wanawasilisha hoja kuomba mahakama iyapeleke Mahakama Kuu kwa ajili ya uamuzi kwa madai yanaathiri kesi.

Alidai notisi hiyo waliwapa Upande wa Jamhuri, wanakusudia kuwasilisha hoja na kwa kuwa washtakiwa hawapo, aliomba kesi iahirishwe, washtakiwa waletwe mahakamani ili hoja hizo ziwasilishwe.

Wakili Kibatala anadai katika notisi kwamba kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza shauri la kikatiba, wateja wao wanaomba ilihamishie suala hilo Mahakama Kuu kwa ajili ya kulitolea uamuzi.

Anadai wakati shauri linatajwa Agosti 9, mwaka huu, Rais Samia alikuwa akihojiwa na Mtangazaji Salim Kikeke wa BBC na kwamba matamshi aliyotoa kuhusu shauri hilo lililoko mahakamani yanaingilia mwenendo wa kesi na yameingia katika mawazo ya jamii kwamba washtakiwa walitenda makosa hayo ya ugaidi.

Katika notisi hiyo inadaiwa kwamba washtakiwa wanaamini mahakama itawatia hatiani kutokana na mazingira hayo na kwamba Rais yuko nafasi ya juu ambapo wengi wanaamini hawezi kuzungumzia suala lililoko mahakamani.

Washtakiwa wanaona hakuna haki itakayotendeka katika shauri hilo kwa kuzingatia kwamba Rais ndiye anayeteua majaji wa Mahakama Kuu na anateua majaji wa Mahakama Kuu kuwa majaji wa Mahakama ya Rufani.

"Rais hawezi kushtakiwa kwa kosa la kuingilia uhuru wa mahakama, alizungumzia suala la kula njama kulipua, kuchoma moto magari, Mbowe kukimbia nchini kukwepa kushtakiwa, kuruka dhamana na alizungumza kama kuna ambaye ameshatiwa hatiani.

"Kikatiba taarifa hiyo inakiuka haki za kikatiba za washtakiwa ambazo zinatakiwa kulindwa, inaonesha hakuna usawa wakati shauri linatakiwa kikatiba liendeshwe kwa usawa kwani ni haki ya washtakiwa kikatiba," inasomeka sehemu ya notisi hiyo.

Mahakama baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, iliamuru washtakiwa wote waletwe siku ya kesi ili kuondokana na shida ya mtandao.

Hakimu Simba alisema inapowasilishwa notisi, kisheria lazima isikilizwe, hivyo mahakama ilipanga kusikiliza hoja zilizomo kwenye notisi hiyo Agosti 27, mwaka huu.

Agosti 6, mwaka huu Jamhuri iliwasomea washtakiwa mashtaka mapya sita, Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwanamizi, Pius Hillar, Christopher Msigwa na Sylvia Mintato.

Upande wa utetezi uliwakilishwa na Peter Kibatala, Lwekamwa Rweikiza, John Mallya, Fredrick Kihwelo, Selemani Makoweka, Michael Rugina, Iddi Msawanga, Jebra Kambole na Sisty Aloyce.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfan Hassan, Adam Kasekwa, maarufu Adamo na Mohamed Lingwenya, ambao wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi namba 63/2020.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka sita. Katika shtaka la kwanza, wanadaiwa wote walikula njama kati ya Mei Mosi na Agosti Mosi 2020 katika Hoteli ya Aishi iliyoko Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro na maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, kulipua vituo vya mafuta kuhatarisha usalama wa taifa na kusababisha hofu kwa jamii.

Katika shtaka la pili, Mbowe anadaiwa katika kipindi hicho na mahali huko, aliwawezesha kifedha Halfani, Adamu na Lingwenya huku akiamini fedha hizo zitasaidia katika kufanya ugaidi kwa kulipua vituo mbalimbali vya mafuta na mikusanyiko kwa lengo la kuharibu misingi ya kisiasa, katiba, uchumi na sifa ya Tanzania.

Washtakiwa Halfani, Adamu na Lingwenya katika shtaka la tatu wanadaiwa kukusanya fedha kutoka kwa Mbowe wakiamini zitasaidia kulipua vituo vya mafuta na mikusanyiko.

Katika shtaka la nne, mshtakiwa Adamu anadaiwa Agosti 5, 2020, eneo la Rau, alikutwa na bastola yenye namba A 5340 aina ya Luger bila kuwa na kibali.

Mshtakiwa Adamu anadaiwa katika shtaka la tano kuwa siku na mahali huko, alikutwa na vilipuzi ambavyo ni risasi tatu bila ya kuwa na leseni.

Mshtakiwa Halfani anadaiwa katika shtaka la sita kwamba Agosti 10, 2020, kwa nia ya kuhatarisha usalama wa nchi, alitumia sare za Jeshi la Wananchi (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kinyume cha sheria.

Anadaiwa kukutwa na suruali moja ya JKT, suruali nne za JWTZ, fulana moja, koti la mvua moja, jaketi moja, kofia tano, overall tano, begi la kubebea vifaa vya JWTZ lijulikanalo kwa jina la ponjoo, vyeo vinne vya koplo, mikanda minne, soksi jozi moja, sweta, begi la mafunzo ya parachuti, kibuyu cha kunywea maji pamoja na kisu aina ya AK 47 CCCP, vyote vya JWTZ.

HABARI KITAIFA

# Sabaya awataja JPM, Mpango

Na Allan Isack, ARUSHA

MKUU wa zamani wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amewataja aliyekuwa Rais, hayati Dk. John Magufuli na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango katika utetezi wake dhidi ya kesi inayomkabili ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Sambamba na viongozi hao wakuu wa serikali kwa nyakati tofauti, pia amemtaja Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, kwamba walikuwa wanafahamu kazi aliyotumwa.

Licha ya kuwataja viongozi hao wenye nyadhifa kubwa serikalini na taasisi nyeti, Sabaya (34), aliwakana washtakiwa wenzake, Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38) akidai kuwa hajawahi kuwaona katika maisha yake zaidi ya kukutana mahakamani kwenye kesi inayowakabili.

"Aliyekuwa Rais hayati Dk. John Magufuli, alinipa agizo la kwenda kufanya kazi maalumu katika duka la Mohamed Saad, lililoko eneo la Soko Kuu jijini Arusha, nikiwa nimeambatana na watu wanne ambao walitumwa kujiunga na mimi kutekeleza agizo la mamlaka yangu ya uteuzi," alidai Sabaya.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, Sabaya alidai kabla na baada ya Februari 9, mwaka huu, alikuwa mtumishi wa serikali katika nafasi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai kwa kuteuliwa na Hayati Rais Magufuli, Julai 29, 2018, nafasi ambayo alidumu nayo kwa miaka miwili na miezi 10 hadi Mei 13, mwaka huu.

Sabaya alidai kuwa licha ya majukumu yake ya kusimamia shughuli za maendeleo, kuhakikisha ulinzi na usalama katika wilaya kutokana na nafasi yake ya mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama, pia alikuwa na kazi ya kutekeleza majukumu yote aliyoagizwa na Rais wa nchi kwa mujibu wa kiapo cha utii.

Pamoja na kukoma utumishi wake Mei 13, mwaka huu, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kutoa tangazo la kusimamishwa kwenye nafasi hiyo kupisha uchunguzi dhidi ya tuhuma mbalimbali zilizokuwa zikimkabili, kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997, bado anabaki na hadhi yake ya utumishi wa serikali.

Alidai kwamba Februari 9, mwaka huu, alikuwa mji mdogo wa Bomang'ombe makao makuu ya Wilaya ya Hai, akiongoza kikao cha kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya kuanzia saa 3:30 asubuhi hadi saa 2:00 mchana.

### ADAI KUTUMWA

Baada ya kumaliza kikao hicho, alidai kuwa majira ya 8:45 mchana, alipokea simu kutoka mamlaka iliyomteua akitakiwa kwenda kutekeleza majukumu aliyopangiwa.

"Mamlaka ya uteuzi ilinipa kazi ya kwenda kufanya kazi Arusha na iliniambia kwamba kuna watu wengine wameshashuka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, hivyo nikaungane nao kwenda kutekeleza kazi hiyo.

"Baada ya kupewa maagizo hayo nilifanya utaratibu wa kutafuta gari la kuwasafirisha watu hao kwenda Arusha kwa ajili ya kazi hiyo na walikuwa na vielelezo vyote vya maelekezo ya sehemu tutapokwenda kuifanya na magari yalikuwa mawili kwenda Arusha," alidai.

Sabaya alidai kuwa watu waliokuwa wametumwa kwenda kuungana naye kwa kazi hiyo walikuwa wanne na walifika Arusha saa 11: 45 jioni na baada ya kufika wakiwa na vielelezo, walikwenda sehemu husika ambayo walielekezwa kufanya mahojiano na mtu wa sehemu hiyo.



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akishuka kwenye gari la Magereza, kwenda kusikiliza kesi inayomkabili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha jana. **PICHA: ALLAN ISACK**

Hata hivyo, aliiomba mahakama kutokuwataja majina watu ambao alifuatana nao kwenye operesheni hiyo kwa madai kuwa hawausiki kwenye mashtaka na kwamba walitumwa kwenye operesheni maalumu na mamlaka iliyowaagiza.

"Eneo husika lilikuwa mtaa wa Soko Kuu na mtu huyo hatukumkuta japokuwa watu hao walikuwa na taarifa zake. Siku hiyo alikuwa dukani na baada ya kutomkuta, niliwasiliana na mamlaka iliyotupa maelezo na walituelezа kwamba wameshawasiliana na Mkuu wa Wilaya ya Arusha kumwambia kwamba watu waliokuwa dukani wakamatwe na kupelekwa kituo cha polisi kwa kuwa watakuwa msaada wa kumpata mmiliki wa duka.

"Huyo mtu ambaye tulikuwa tukimtafuta anaitwa Mohamed Saad Hajirini. Tulitekeleza agizo hilo kwa kuwakamata watuhumiwa kuwapeleka polisi na baada ya hapo nilimjulisha DC (Mkuu wa Wilaya) wa Arsha kwamba maelezo mengine alishajulishwa," alidai.

Sabaya alidai kwamba watu hao waliowakamata kuwapeleka polisi hawafahamu majina yao, lakini walikuwa wauzaji na hawakuwa wamiliki bali mmiliki walikuwa wanamfahamu.

"Mimi nilitumwa kutoka Hai kwenda Arusha kufanya kazi hiyo. Mwenye jibu au sababu kwa nini mimi siyo mwingine ni mamlaka iliyoniteua na kunipa kazi hiyo. Pia kutoka Hai hadi Arusha ni karibu sana na haikuwa kazi ya kwanza kuifanya kwa sababu miezi michache tulikamata mitambo inayotengeneza noti bandika nchini, Chanika mkoani Dar es Salaam, nikiwa kiongozi wa kikosi hicho na Gavana wa BoT na Makamu wa Rais wa sasa, Dk. Philip Mpango, akiwa Waziri wa Fedha, wanafahamu tukio hilo," alidai. Aidha, alidai kwamba alipokuwa akipewa kazi ya operesheni maalumu alikuwa anashirikiana na vyombo vyote vya dola vilivyoko ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kuhusu madai ya kuvamia duka, kuiba Sh. 276,000 kisha kuwapiga Numan, Bakari Msangi, Salim Hassan na Ally Shabani kwa kutumia silaha kuwatishia ili kutimiza azma yao, Sabaya alidai si kweli.

### AWAKANA WENZAKE

Kuhusu washtakiwa wenzake, Nyegu na Mbura, Sabaya alidai kuwa hawafahamu na hakuwahi kuwaona wala kukutana nao katika maisha yake.

Kuhusu tuhuma za kuiba, alidai: "Sizifahamu wala hazinihusu. kwa bahati nzuri hakuna mtu yeyote aliyesema ameniona nikiiba fedha hizo kati ya waliokuja hapa mahakamani kutoa ushahidi.

"Kwa ushahidi wa mashahidi 11 wa mashtaka, hakuna shahidi aliokuja kuzungumzia tukio la wizi Februari 9, mwaka huu na badala yake wanazungumzia Februari 12 mwaka huu, na sijatajwa na popote kuhusu hizo bunduki."

Pia alidai kuwa Numan na Bakari Msangi hawafahamu majina yao bali amewajua mahakamani, wakidai kwenye ushahidi wao na hakuna sehemu walipodai kuwa Februari 9 walitishiwa na kunyang'anywa fedha

Kadhalika, alidai kwamba Bakari Msangi hakumwona, hakupigwa wala kukutana naye popote na alichoieleza mahakama ni uongo na hujuma za kisiasa dhidi yake na kwamba hakuwahi kumtishia silaha na kumnyang'anya Sh. 390,000.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**Mahakama ya mwanzo ya MAILI MOJA**
**Wilaya ya KIBAHA**
**MADAI NAMBARI 75 YA 2021**
**Mdai ACCESS MICROFINANCE BANK TZ (AMEDIUS MALLY) Mdai**
**Mdaiwa KBM & SONS COMPANY LTD**
**Kwa KBM &SONS COMPANY LTD/MKURUGENZI WA MWENGE DSM**
**Kwa kuwa mdai / wadai wameleta / ameleta madai yake / yao kwamba**
**MADAI YA SH.6,000,000/= MILIONI SITA ELFU TU.**

Kwahiyo anahitajika/mnahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya tarehe 10/09/2021 saa 2:30 asubuhi kwakujibu madai hayo na kwakuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwaajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria au hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu ,mahakama ikithibitika kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini hii.itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe ….20…



216408402

# Bunge lawaweka matatani vigogo wa halmashauri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imeziweka matatani halmashauri mbili za Chamwino na Chemba mkoani Dodoma baada ya kuagiza kufanyika ukaguzi maalum ili kujiridhisha kuhusu matumizi ya fedha kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Grace Tendega, alitoa agizo hilo jana jijini Dodoma wakati akiwasilisha maagizo ya kamati kwenye majumuisho ya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyofanyika katika Wilaya za Mpwapwa, Chamwino na Chemba.

Tendega aliiagiza Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) kufanya ukaguzi maalum kwa halmashauri hizo katika miradi ya maendeleo ambayo kamati haijaridhishwa na utekelezaji wake.

Alibainisha kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, ukaguzi huo ufanyike kwenye miradi yote ya maendeleo iliyotekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 na 2019/20.

Alisema ukaguzi huo maalum utasaidia kupata majibu kutokana na kamati yake kutoridhishwa na utekelezaji wa miradi.

"Lengo kuu la ukaguzi huo ni kubaini nidhamu ya fedha iliyokuwapo katika matumizi ya fedha za umma, tija iliyopo katika miradi iliyoibuliwa na kutekelezwa na kutoa mapendekezo ya hatua stahiki kwa watakaobainika na ubadhirifu au ukiukwaji wa matumizi ya fedha za umma," alisema.

Tendega alisema kamati hiyo imeiagiza Chemba kutumia fedha zake za ndani kukamilisha ujenzi wa bweni la shule kabla ya Januari mwakani, akibainisha kuwa hadi sasa kiasi cha Sh. milioni 97 kimetumika lakini bado halijakamilika.

"Jengo halina ubora, kuta zake tayari zimeshaanza kupinda kuashiria udhaifu wa usimamizi wa kitaalamu kutoka hatua za awali hadi hapo ulipofikia," alisema.

Aliongeza kuwa katika ujenzi wa bweni hilo la wanafunzi, serikali ilitoa kiasi cha Sh. milioni 80 kama ruzuku, nguvu za wananchi Sh. milioni 17 na mchango wa halmashauri ni Sh. milioni saba.

"Pamoja na kiasi hicho cha fedha, lakini bado Halmashauri ya Chemba inaomba iongezewe kiasi cha Sh. milioni 23 ili imalize ujenzi wa bweni yaani jumla itakuwa ni Sh. milioni 127, sasa kamati inaagiza kuwa halmashauri kutumia fedha zake za ndani kukamilisha ujenzi huo kabla ya Januari 2022," alisema.

Tendega alisema kamati hiyo inaagiza halmashauri hiyo kutumia fedha zake za ndani kujenga sakafu ya madarasa mawili pamoja na kufunga taa ambazo zinawezesha wanafunzi kujisomea wakati wa usiku.

"Agizo hili linatakiwa kutekelezwa kabla ya Desemba mwaka huu, kamati itajiwekea utaratibu wake kwenda kukagua agizo hilo," alisema.

Vilevile, kamati hiyo imeutaka uongozi wa Halmashauri ya Chemba kufuatilia kiasi cha Sh. milioni 250 kilichorudishwa Hazina baada ya mwisho wa mwaka fedha 2020 kilikuwa sehemu ya fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya unaogharimu Sh. bilioni 1.5.

"Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chemba ulitengewa Sh. bilioni 1.5, kiasi kilichotumika ni Sh. bilioni 1.55, kiasi cha Sh. milioni 250 kilirejeshwa Hazina baada ya mwisho wa mwaka Juni 30, 2020," alisema.

Tendega alisema mpaka sasa majengo saba yamekamilika kwa zaidi ya asilimia 90, isipokuwa wodi ya watoto na kinamama na kiasi cha Sh. milioni 72 kililipwa kwa makandarasi bila tathmini ya kazi iliyofanyika.

Kuhusu Chamwino, mwenyekiti huyo alisema ukaguzi huo maalum ufanyike kwenye ujenzi wa bweni na bwalo la Shule ya Sekondari Mvumi Mission ili kubaini namna fedha zilivyotumika na kutoa mapendekezo ya hatua stahiki.

Tendega alisema ujenzi wa bwalo katika shule hiyo umegharimu Sh. milioni 100, lakini ujenzi wake umefikia asilimia 30.

"Kamati pia imebaini usimamizi mbovu wa fedha kulipwa bila uthibitisho wa mkurugenzi katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya iliyoko Mlowa barabarani na kwa mujibu wa kitabu cha wageni, kamati imebaini mkurugenzi hajawahi kufika hata mara moja toka ujenzi huo uanze," alisema.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, aliahidi kufanyia kazi maelekezo ya kamati hiyo na kuunga mkono kufanyika kwa ukaguzi huo.

"Na hicho ndicho kigezo changu ambacho wakurugenzi watanishawishi ili niweze kumweleza Rais kuwa wanafaa kuendelea kuwa viongozi katika nafasi zao," Ummy alionya.


The Guardian Limited

VACANCY

Freelance Sales Executives

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Zanzibar, Tanga, Morogoro and Kilimanjaro.**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th August, 2021.**

61637602


## Daktari bingwa wa watoto afariki dunia

**Na Romana Mallya**

DAKTARI Bingwa wa Watoto, Augustine Massawe, anayemiliki Hospitali ya Furaha Medical, amefariki dunia katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alikokuwa anatibiwa maradhi yaliyokuwa yakimkabili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na uongozi wa Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Dk. Massawe alifariki dunia jana hospitalini huko.

"Tunasikitika kutangaza kifo cha Dk. Massawe kilichotokea leo Agosti 13 Hospitali ya Muhimbili, Dk. Massawe alikuwa Mhadhiri Mwandamizi katika Idara ya Watoto (Pediatrics and Child Health) Skuli ya Tiba," taarifa hiyo ilibainisha.

Uongozi wa chuo hicho ulisema msiba uko nyumbani kwa marehemu Mbezi Beach na mipango ya mazishi inaendelea kuratibiwa na ratiba kamili itatolewa mara itakapokamilika.

Dk. Massawe amekuwa akitibu watoto tangu mwanzoni mwa miaka ya 1980 na taarifa za kifo chake zimepokewa kwa hisia tofauti na baadhi ya wanawake ambao watoto wao waliwahi kutibiwa na mtaalamu huyo, wakisisitiza ni pigo kwa taifa.

Baadhi yao waliandika jana katika mitandao ya kijamii ujumbe mfupi ukiwamo uliosomeka "Mwanangu wa kwanza aliugua sana nikiwa Kigoma, hiyo ilikuwa mwaka 2012, nilihangaika sana hadi nilisafiri kuja Dar es Salaam, nikaenda kwenye hospitali yake akamwona, akamtibu akapona kabisa."

Mwingine aliandika, "Ametibu watoto wengi, kwa kweli tuna shuhuda naye huyu daktari. Mungu ampe pumziko jema."

Mwombelezaji mwingine aliandika: "Aliwapenda watoto na kuwatibu, alimaanisha kutoka moyoni, hakika Mungu atamlipa, Mungu amrehemu."

## Chuo chaunda helikopta kukabili majanga nchini

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

CHUO cha Ufundi Arusha (ATC) kipo mbioni kukamilisha uundaji wa helikopta ambayo itatumika kufanya uokoaji wakati wa majanga mbalimbali.

Hatua hiyo ya chuo hicho imetokana na maboresho makubwa yaliyofanywa na serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mkufunzi wa Chuo hicho Idara ya Magari, Abdi Mjema, alibainisha hayo jana jijini humo alipozungumza na waandishi wa habari waliopo kwenye ziara ya kuangalia maboresho hayo.

Alisema ubunifu wa helikopta hiyo ulianza mwaka 2015 ukilenga chombo hicho kitumike kwenye uokoaji yanapotokea majanga mbalimbali zikiwamo ajali za moto hasa kwenye maeneo yasiyofikika kwa urahisi hasa milimani.Alisema walitarajia ikamilike na kuanza majaribio ya awali ya kuruka mwishoni mwa mwaka 2018, lakini kutokana na vikwazo mbalimbali, sasa majaribio hayo yatafanyika mwakani.

"Magari yamekuwa yakitengenezwa na wabunifu mbalimbali, sasa sisi tukaona tuende mbali zaidi kwa kuwa teknolojia ya kurusha ndege sio uchawi, ni mambo ya kisayansi na kihandisi.

"Tunafanya hivi kwa sababu katika nchi hii kuna majanga yamewahi kutokea ambayo yanahitaji vyombo kama hivi kutumika.

## TANGAZO





betPawa inatoa nafasi kwa wateja wote kuanza msimu mpya wa Ligi kuu ya Uingereza wakiwa na gari mpya.

Mtanzania mmoja atabahatika kujishindia Toyota RAV4 mpya kabisa. Watano watajishindia PS5 na CD ya Fifa 21, na wawili watapata shilingi laki 5 kila mmoja kwa ajili ya shopping Shoppers supermarket.

Tumia nafasi yako kushinda kikubwa ZAIDI, bashiri mechi yoyote ya ligi kuu Uingereza kupitia betPawa na uingie katika droo.

Una nafasi hadi Jumapili ya tarehe 29 Agosti kushiriki na washindi 8 watapatikana katika droo siku ya Jumatatu tarehe 30 Agosti.

Wataalikwa Dar es Salaam katika shindano la upigaji penalti mwezi Septemba.
Mshindi ataondoka na Toyota RAV4, na hakuna mtu ataondoka bila zawadi.

Je utakua mshindi? Unaweza kushiriki kwa kubashiri kwa kiwango kidogo cha TSH 1 tu.

Tukutane sheli na betPawa!
Ingia **betpawa.co.tz/epl-launch-giveaway**

betPawa

Cheza kiasi. 18+. betPawa imesajiliwa chini ya bodi ya michezo ya kubashiri ya Tanzania. Leseni #SBI000000026.

216408301

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usajili wachezaji wapya uende sawa na mazoezi

**TIMU** mbalimbali zinazotarajiwa kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/22 zinaendelea na mchakato wa kusajili wachezaji wapya kwa ajili ya kuboresha na kuimarisha vikosi vyao.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lilitangaza dirisha la usajili litafungwa rasmi Agosti 31, mwaka huu, lakini timu zinazoshiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Mchezo huo Afrika (CAF), zenyewe zinatakiwa kukamilisha mchakato huo hapo kesho Jumapili.

Huku tayari TFF imeshatangaza msimu mpya utaanza ifikapo Septemba 29, mwaka huu, lakini ukifunguliwa na mchezo wa Ngao ya Jamii utakaochezwa Septemba 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kwa kuwakutanisha watani wa jadi, Simba na Yanga.

Kwa sasa kila timu imekuwa ikiendelea na mchakato wa kusajili wachezaji wapya ambao inaamini watasaidia kuongeza nguvu katika timu zao kwa kuzingantia mapendekezo kutoka kwa makocha wao, lakini ikiwaacha nyota ambao inaamini hawapo kwenye mipango yao.

Tunazikumbusha timu zote kuendelea kusajili kwa kuzingatia mahitaji halisi na kuacha kufuata 'mkumbo' kwa kuangalia wapinzani wao wanachofanya, kwa sababu kwa kufanya hivyo hawatafikia malengo yao na huko mbele wakajiweka kwenye hatari ya kushuka daraja.

Nipashe inazikumbusha timu zote mbali na kusajili, wanatakiwa pia kuwapa wachezaji hao maandalizi sahihi kulingana na ushindani wa ligi na mashindano yote watakayoshiriki.

Baadhi ya timu ambazo hupata matokeo mabaya katika mechi zao za ufunguzi, zimekuwa ya kulalamika kukosa maandalizi bora ikiwamo kucheza mechi za kirafiki na hivyo kuanza msimu mpya wakati wachezaji wao hawajafahamiana vyema au wamekosa kile wanachoita muunganiko.

Wamiliki wa timu wanatakiwa wakumbuke pia kuboresha mabenchi yao ya ufundi na kuacha tabia ya kuajiri kocha mwenye sifa, lakini anayezungukwa na wasaidizi ambao hawana elimu iliyojitosheleza na matokeo yake hushindwa kutoa msaada pale Kocha Mkuu anapoelemewa.

Huu ndio wakati wa makocha kuhakikisha programu zao zinatekelezwa vyema na kuondoa malalamiko baada ya kipenga kuanza kwa sababu kila timu inakuwa imepata muda sahihi wa kujiandaa.

Sio lazima kila timu inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara iweke kambi nje ya nchi, timu zinaweza kujipanga kwa kuandaa kambi yake hapa hapa nyumbani, lakini kwa kuhakikisha programu zote zinatekelezwa na hatimaye kufikia malengo waliyojiwekea katika msimu mpya unaokuja.


Kujiandaa vyema ndio kutaifanya timu iweze kupata matokeo chanya katika mechi zake, lakini ikivuna pointi nyingi kwenye mzunguko wa kwanza ambao hutoa taswira ya timu zitakazokuwa kwenye mbio za ubingwa na zile zitakazobakia kupambana kujinasua kutoshuka daraja.

Huu ni wakati mwingine kwa wachezaji kujitambua kwa sababu atakayefanikiwa kuonyesha kiwango kizuri, atajiweka kwenye nafasi nzuri ya kupangwa katika kikosi cha kwanza cha timu yake, lakini pia kuendelea kukitangaza kipaji chake kwa klabu nyingine za ndani na nje ya Tanzania.

Mchezaji atakayejituma na anayetumia vizuri kipindi hiki cha maandalizi ya msimu, atakuwa amejiimarisha na hapo atajitengenezea njia ya kuitwa katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambacho kocha wake mkuu, Kim Poulsen huifuatilia hiyo kwa karibu ligi hiyo ya juu nchini.

Bingwa wa ligi au mafanikio katika soka hupatikana kwa timu iliyojiandaa vyema na si jambo lingine lolote la nje ya uwanja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Chako ni chako...



Na Barnabas Maro

**"CHAKO** ni chako cha mwingine sio chako." Maana yake kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa tena una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine.

Twafunzwa tuvitegemee vitu vyetu wala sio vya watu wengine. Pia hutukumbusha kuvithamini vitu vyetu ingawa sio vizuri kama vya wengine. Sizungumzii vitu bali nazungumzia watu, hasa wacheza kandanda/kabumbu wetu wa Tanzania.

"Bura yangu sibadili na rehani (debwani)." Maana yake kitamba changu duni (bura) sibadili na kingine cha thamani kubwa (rehani) methali hii yatufuza tutosheke na vitu vyetu kwa kuwa vina faida kwetu kuliko vya watu wengine ambavyo haviwezi kutufaidi.Tusividharau vitu vyetu hata kama ni vibaya.

Wachezaji wanaoingia uwanjani kucheza kandanda huwa 11 mbali ya wachezaji wa akiba wanaokuwa nje ya dimba kusubiri jambo litakalomsibu mchezaji yeyote atakayepangwa mchezoni na atakayetolewa uwanjani ama kwa kuumia, kutolewa nje ya uwanja kwa kadi nyekundu au anayeshindwa kucheza kama atakavyo mwalimu.

Timu zinaruhusiwa kusajili wachezaji 10 wageni kutoka nje ya Tanzania. Kuna wakati timu zenye wachezaji wengi wa kigeni huchezesha wageni wapatao 7 ilhali wenyeji ni 4 tu! Hivi kweli Tanzania yenye zaidi ya watu milioni 54 na ushei (na ziada na zaidi kidogo) inakosa wachezaji hata ilazimike kuchukua wachezaji wengi kutoka nje ya nchi?

Twapaswa kutambua kuwa "Si kila mwenye kucha huwa samba." Maana yake sio wanyama wote wenye makucha huwa simba. Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu anayejidai kuwa na sifa au uwezo ambao hana.

Wallahi (kwa jina la Mwenyezi Mungu) wachezaji wageni wanaosajiliwa humu nchini na Simba na Yanga huwaambia wezao huko kwao, kuwa wachezaji wa kigeni wanalipwa mishahara mikubwa kuliko wanayolipwa huko kwao. Kwa hiyo huwa tayari wakati wote kujiunga na timu za nje hasa za Yanga, Simba na Azam FC, za Dar es Salaam. Naam, Bandari ya Salama!

Ni wangapi waliokuja Tanzania lakini wakashindwa na wenyeji kisha wakawekwa nje ya uwanja wakati wachezaji wenyeji wakicheza vizuri kuliko wageni waliletwa kwa mbwembwe na kulipwa mishahara mikubwa kuliko wachezaji wenyeji? Hali hiyo huwafanya wachezaji wetu kucheza kwa manung'uniko ya kimoyomoyo.

**"Bura yangu sibadili na rehani (debwani)." Maana yake kitamba changu duni (bura) sibadili na kingine cha thamani kubwa (rehani) methali hii yatufuza tutosheke na vitu vyetu kwa kuwa vina faida kwetu kuliko vya watu wengine ambavyo haviwezi kutufaidi.Tusividharau vitu vyetu hata kama ni vibaya.**

Kama Tanzania ina vijana wengi wenye uwezo wa kusakata gozi la ng'ombe, kwa nini Serikali isiwe na shule maalum ya vijana kujifunza kandanda ili timu zetu zinapotaka wachezaji ziwachukue kutoka huko na kupatiwa fedha wanazolipwa na timu zinazohitaji wachezaji kutoka huko?

"Mwenye busara mara hunasihika." Maana yake mtu mwenye hekima hufuata ushauri apewao. Hutumiwa kutukumbusha umuhimu na faida za kuyafuata mashauri tunayopewa na wazazi wetu au na watu wanaotuzidi maarifa.

Kwa Simba na Yanga nawaambia: "Mchimba kisima huingia mwenyewe." Maana yake mtu anayemchimbia mwingine shimo kwa dhamira mbaya huishia kuingia yeye mwenyewe.

Methali hii huweza kutumiwa kumshauri mtu anayemfanyia mwenzake ubaya, kuwa huenda ubaya huo ukamrudia yeye.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

HABARI KITAIFA

## Kipande cha barabara km 50 sasa kukamilika Desemba

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imesema barabara ya Makutano – Butiama – Nyamuswa sehemu ya Makutano – Sanzate yenye urefu wa kilomita 50, ujenzi wake kwa kiwango cha lami utakamilika Desemba, mwaka huu.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Dk. Leonard Chamuriho, alisema hayo jana mkoani Mara wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa barabara hiyo inayojengwa kwa ushirikiano wa makandarasi wazawa 10.

Chamuriho alisema mradi huo unaojengwa na Mbutu Bridge JV kwa kushirikiana na makandarasi wengine tisa, umechelewa kukamilika kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kubadilika mara kwa mara kwa michoro ya barabara na pia makandarasi kuwa na uwezo mdogo wa kifedha na vifaa.

"Wananchi wa mkoa wa Mara, sasa tutarajie neema katika mkoa huu. Barabara hii iko ukingoni kukamilika. Changamoto zilizokuwa zikikabili mradi huu zote zimekwisha, hivyo matumaini yangu kuanzia sasa kazi zitafanyika kwa haraka na mradi utakamilika kwa wakati," alisema.

Pia Waziri Chamuriho alisema kukamilika kwa barabara hiyo kutasaidia kupunguza gharama za usafirishaji kutoka eneo moja kwenda lingine na pia kutachochea biashara ya utalii kwenye mbuga za wanyama za Serengeti na Ngorongoro.

Mbunge wa Butiama, Jumanne Saghini, alisema anashangazwa na ujenzi wa barabara hiyo kuchukua muda mrefu, hivyo kuiomba serikali kumbana mkandarasi ili kumaliza mradi huo kwa wakati na hatimaye wananchi wafurahie usafiri na usafirishaji kama watu wengine.

Naye Mbunge wa Bunda, Mwita Getere, aliiomba serikali kuhakikisha inamkumbusha mkandarasi kuweka alama za barabarani ili kusaidia masuala ya kiusalama kwa watumiaji wa barabara hiyo.

Katika hatua nyingine, Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Mara, Mhandisi Ngaile Mlima, alisema mradi huo umefika asilimia 89 na kazi ambazo zimeshafanyika ni pamoja na uondoaji wa tabaka la juu la udongo, upasuaji miamba na kujenga tuta kwa tabaka la chini.

# Umaskini wapungua kwa asilimia 12

Na Elizabeth John, NJOMBE

UMASKINI wa mahitaji ya msingi kwa kaya za walengwa wa mapango wa kunusuru kaya maskini umepungua kwa asilimia 10 na umaskini uliokithiri umepungua kwa asilimia 12.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Ladislaus Mwamanga, wakati wa kikao kazi cha kujenga uelewa kuhusu sehemu pili ya awamu ya tatu ya TASAF katika utekelezaji wa mpango huo.

Alisema mafanikio hayo yamepatikana kutokana na walengwa kujikita kwenye shughuli za kukuza kipato na kujiimarisha kiuchumi.

"Kaya za walengwa zimekuwa zikifanya shughuli mbalimbali zikiwamo kilimo, ufugaji, uvuvi na mradi ya ujasiriamali. Haya ni mafanikio makubwa ambayo yanatakiwa kulindwa ili kaya hizi zisirudi kwenye hali ya umaskini," alisema Mwamanga.

Pia alisema maeneo yote ambayo hayakufikiwa katika kipindi cha kwanza yatafikiwa katika kipindi cha pili.

"Nawajulisha kuwa maeneo ambayo hatukufika kipindi cha kwanza, muda umefika. Katika kipindi hiki cha pili tutafika katika vijiji na mitaa yote Tanzania Bara pamoja na shehia zote za Unguja na Pemba kwa Zanzibar," alisema Mwamanga.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF kitafikia kaya milioni 1.45 zenye zaidi ya watu milioni saba na kwamba mpango huo umelenga kusahihisha changamoto zilizojitokeza awamu zilizopita ikiwamo kuhusisha watu wenye ulemavu.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Marwa Rubirya, ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema viongozi wanapaswa kukemea vitendo vya upendeleo katika mpango wa TASAF.

"Nisisitize kwenye utambuzi sisi viongozi tunao wajibu wa kuhamasisha walengwa kuanzisha miradi ya ujasiriamali ambayo itawasaidia kukuza vipato vya kaya lakini kujiwekea misingi bora na ikitokea fedha hizo zimetumika tofauti na malengo, basi kutolewe maelekezo mahususi ili fedha hizo zitumike kama ilivyopangwa," alisema Rubirya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Sharifa Nabarang'anya, aliwataka waratibu wa TASAF ngazi ya halmashauri kufanya kazi kwa weledi, kuondoa kaya hewa sambamba na kutoa elimu kwa walengwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Valentino Hongoli, aliipongeza TASAF kwa mchango wao wa kuinua maisha ya wananchi katika kata zao ikiwamo kuwapelekea miradi ya ujenzi wa madarasa katika shule za msingi na sekondari.



Ofisa Msimamizi wa Chama cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA), Mkoa wa Arusha, Mohamed Mpinga (kulia), akizungumza na baadhi ya madereva wa daladala wa jijini Arusha juzi akiwataka kuchukua tahadhari zote za kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walia uendeshaji mwendokasi, kujazwa abiria

Na Mwandishi Wetu, PEMBA

BAADHI ya abiria wanaotumia magari ya Chake Chake- Muambe na Mkoani-Muambe mkoa wa Kusini Pemba wamelalamikia madereva kwa kuendesha mwendo kasi na kupakia kupita kiasi.

Wamesema jambo hilo linawakwaza na hata kuhatarisha usalama wao wanapokuwa safarini.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hii jana, abiria hao walisema kuwa madereva wamekuwa wakiendesha magari kwa mwendokasi hali ambayo inawasababishia wakati mwengine kutaka kuahirisha safari wakiwa njiani.

Kwa mujibu wa abiria hao hali hiyo inasikitisha kwa kuwa madereva hao wanatumia vibaya vyombo hivyo kwa kuwatia hofu abiria wakiwa kwenye safari kwa vile wengine hukaribia kukumbwa na shinikizo la damu.

"Tulio wengi tuna magonjwa ya moyo halafu magari wanaendesha wanavyotaka wao. Kwa kweli inatuuma sana, tunaomba wapunguze mwendo," alisema mmoja wa abiria aliyekuwa akisafiri kutoka Chakechake kwenda Muambe.

Kwa mujibu wa abiria huyo, tabia ya kuwachukua abiria na kuwajaza ndani ya gari kama machungwa, inahitaji kuondoshwa kwa kuwa inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza.

"Kama siku hizi tunaambiwa kwamba ugonjwa wa corona upo na unaenea kwa njia ya hewa, hivyo kwa abiria tunavyojazwa kwenye magari, hatuwezi kusalimika ikiwa kuna mmoja wetu ana maambukizi ya ugonjwa huo," alisisitiza abiria huyo.

Licha ya kuwajaza abiria na kuendesha kwa mwendokasi, abiria huyo alisema pia madereva hao wamekuwa na tabia ya kuwadhalilisha wanawake, watoto na wasiojiweza kwa kuondosha gari kabla hawajakaa.

"Wanatuangusha na sijui wanakimbilia nini? Huu ni udhalilishaji wanaotufanyia kwa sababu mtu mzima anaanguka chini. Tunaiomba serikali itusaidie," alisema. Naye Asha Ali Abdalla (si jina lake halisi) alisema barabarani huwapo askari ingawa hawaoni kuchukua hatua yoyote licha ya magari hayo kujaza sana na kuendeshwa kwa mwendokasi.

"Huwa najiuliza hivi hawa askari hawazioni hizi gari au wanaelewana na madereva, kwa sababu kila siku tunapiga kelele lakini hali ndio hiyo hiyo," alisema.

Mmoja wa madereva ambaye hakutaka kutajwa jina lake litajwe, alikiri kuwa ni kweli baadhi ya madereva huendesha magari kwa mwendokasi, ingawa wengine wanajitahidi kwenda mwendo wa kiasi.

"Barabara ni mbovu sana kwa hiyo hata ukienda kwa mwendo mdogo inaonekana mwendo wa kasi kutokana na mashimo yaliyoko barabarani," alisema dereva huyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, Richard Mchomvu, alikiri kuwapo kwa hali hiyo na kusema madereva wenye tabia ya kuendesha kwa mwendokasi pamoja kujaza abiria kwenye magari kama mizigo wataendelea kusakwa na kuwajibishwa kisheria.

"Wanakwenda mwendo wa kasi wala hawajali kwamba wamebeba watu wenye uhai na wenye shughuli zao, hivyo hawa tutawachukulia hatua za kisheria tutakapowakamata," alisema Mchomvu.

Aliwataka madereva hao kuacha tabia ya kujaza abiria kupita kiasi ili kuepuka kuambukizana magonjwa ikiwamo corona.

Pia aliwataka wananchi kutoa taarifa polisi pale wanapokuta matendo hayo na kusema watahakikisha wanadhibiti hali hiyo ili kuepusha majanga.

# Watekeleza agizo la PM upandaji michikichi

**Na Ashton Balaigwa, KIGOMA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kasulu na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, zimeitikia agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa la kuendeleza kilimo cha michikichi baada ya kupanda ekari 1,959.95 katika maeneo yenye fursa ya kilimo hicho.

Hadi kufikia Juni, mwaka huu, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ilipanda ekari 1,509.95 huku Kasulu ikipanda ekari 450 na kuanza maandalizi ya kupanda ekari 2000 zaidi.

Akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea mashamba hayo kujionea utekelezaji wa agizo hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Joseph Kashushura, alisema miche hiyo ambayo ni 22,620 aina ya Tenera imepandwa katika mashamba ya wakulima na taasisi 16 za serikali na zisizo za kiserikali.

Alisema halmashauri imedhamiria kuongeza uzalishaji wa michikichi katika mwaka wa fedha wa 2021/22 na imeamua kutenga Sh. milioni 53 kwa ajili ya kuanzisha eneo jipya ambalo litakuwa na ekari 2,000.

"Sisi Halmashauri Wilaya ya Kasulu katika kutekeleza agizo la Waziri Mkuu, tumedhamiria kufanya kilimo cha michikichi kwa ajili kufanya biashara ya kuzalisha mafuta ya kula. Licha ya kupanda ekari 450, tumeamua kwa dhati kuanzisha eneo la kilimo kwanza lenye ekari 2,000 kwa ajili ya zao hilo," alisema.

Naye Kaimu Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Ramadhani Amri, alisema katika kuitikia agizo la Waziri Mkuu wameshapanda miche 86,065 ya aina ta tanera karika ekari 1,509,950 kwa wakulima 1, 129 na wakulima binafsi 1,121 pamoja na taasisi nane.

Alisema halmashauri hiyo imezalisha miche 32,665 wakati miche 53,400 ilitolewa na taasisi mbalimbali zikiwamo za Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Kihinga mkoani Kigoma.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alizipongeza halmashauri hizo kwa kuitikia agizo hilo kwa kuendeleza kilimo cha michikichi ambacho kinatoa fursa za kuzalisha mafuta ya kula.

Dk. Mkamilo alisema TARI imefanya utafiti na kuja na mbegu aina ya tenera ambayo ina sifa ya kuongeza uzalishaji wa mafuta tani tano mpaka sita ambayo imegawiwa bure kwa wakulima katika mkoa wa Kigoma ili kuendeleza zao hilo na kusaidia kuzalisha mafuta ya kula.




Ofisa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Glory Khahima (wa tatu kulia), akitoa maelezo kwa walipa kodi wapya waliofika hapo kwenye kampeni ya kusajili walipa kodi wapya katika eneo la Goba, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mfumo kidijitali warahisisha usajili BRELA

**Na Mwandishi Wetu, CHATO**

WAKALA wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA), umerahisisha utoaji wa leseni kutokana na wafanyabiashara kujisajili kwa njia ya mtandao badala ya kusafiri umbali mrefu kwenda kwenye ofisi za taasisi hiyo.

Ofisa Msaidizi wa Usajili wa BRELA, Seleman Seleman, alisema hayo jana mjini hapa wakati akimfafanulia jambo Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe.

Mwambe alitembelea tamasha la kuhamasisha utalii na maonyesho ya biashara linaloendelea Chato mkoa wa Geita kwa lengo la kukuza biashara na utalii.

"Hivi sasa mtu yeyote anayehitaji huduma zetu haina haja ya kusafiri kuja ofisini. Usajili unafanyika kwa njia ya mtandao ukiwa popote na muda wowote," alisema.

Seleman na kuongeza kuwa licha ya kutoa huduma kwa njia ya mtandao, BRELA imechukua hatua zaidi kwa kuwafuata wafanyabiashara katika maeneo yao na kuwapatia huduma za papo kwa papo.

Aidha, Suleman alitoa wito kwa wakazi wa mkoa wa Geita na jirani kutumia fursa hiyo kufika katika maonesho hayo ili kupata elimu na usaidizi wa haraka.

Selemani alisema katika maonesho hayo ili kufanya usajili wa papo kwa papo, wadau wanatakiwa kufika na namba ya kitambulisho cha taifa, namba ya simu inayofanya kazi na anuani ya barua pepe inayofanya kazi.

Alisema kwa wale ambao wametuma maombi ya huduma mbalimbali na bado hayajakamilika, wanahimizwa kufika katika banda la BRELA ili kupata maelekezo na usaidizi wa haraka wa kukamilisha maombi yao.

Ofisa huyo alisema katika maonyesho hayo, huduma zingine zinazotolewa ni pamoja na usajili wa kampuni, majina ya biashara, alama za biashara na huduma, kupata leseni za biashara kundi A.

Alisema tamasha la kuhamasisha utalii na maonyesho ya biashara lilianza Agosti 7 na kuzinduliwa rasmi na Waziri Mwambe na linatarajiwa kufikia tamati Agosti 15, mwaka huu.

Katika hatua nyingine, wafanyabiashara washiriki wa tamasha hilo waliipongeza BRELA kwa huduma wanayotoa katika maonyesho hayo.

Haliswa Chobba ambaye ni mfanyabiashara na mshiriki wa maonyesho hayo akitokea Dar es Salaam aliyesajili jina la biashara papo kwa papo, alisema amefurahishwa na huduma aliyopata BRELA tangu amefika katika banda hilo na kufanikiwa kupata cheti cha usajili.

# Mrundikano wanafunzi Kibaha kuwa historia

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

TATIZO la mrundikano wa wanafunzi katika Shule ya Msingi Mtongani, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, liko mbioni kumalizika baada ya kukamilika kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa na ofisi ya walimu.

Ujenzi wa majengo hayo ambayo umegharimu Sh. milion 100 umeondoa kero kwa wanafunzi ambao awali walikuwa wanakaa zaidi ya 50 katika chumba kimoja cha darasa.

Mradi huo wa ujenzi ambao umetekelezwa kwa kutumia utaratibu wa 'force account', umegharimu Sh. milioni 100 ni kwa majengo na samani zake.

Akizungumza baada ya kuzindua mradi huo juzi, kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Luteni Josephine Mwambashi, aliwataka watendaji kuwa wazalendo wakati wa kusimamia miradi hiyo ya maendeleo inayowasaidia wananchi.

Pia aliwataka viongozi kwenye halmashauri ambazo mwenge huo utapita kubakikisha wanawasilisha taarifa za miradi mapema kwa wakimbiza Mwenge ili zianze kupitiwa kabla ya kufika kwenye maeneo ya miradi.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sarah Msafiri, alimwomba kiongozi huyo kuwakabidhi wakurugenzi wa Halmashauri za Mji Kibaha na Wilaya ya Kibaha madawati 50 ambayo yamenunuliwa kwa fedha za serikali, wahisani na wananchi.

Msafiri alisema madawati hayo yatagawiwa katika shule za msingi Mtongani na Kongowe katika halmashauri hizo.

Akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainab Abdallah, Msafiri alisema Mwenge huo utakimbizwa katika wilaya hiyo kukagua, kuzindua na kuweka mawe ya msingi katika miradi 13 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni mbili.

**Akizungumza baada ya kuzindua mradi huo juzi, kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Luteni Josephine Mwambashi, aliwataka watendaji kuwa wazalendo wakati wa kusimamia miradi hiyo ya maendeleo inayowasaidia wananchi.**



# Ahamasisha wananchi kujiunga bima ya afya

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Emmanuel, amewataka viongozi kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (CHF iliyoboreshwa) ili kuwa na uhakika wa matibabu.

Emmanuel aliyasema hayo jana alipokuwa akizindua ugawaji wa bima hizo kwa wananchi wa Kata ya Mkoka wilayani humo ikiwa ni miongoni mwa kaya 300 zinazoishi katika mazingira magumu zilizogharamiwa bima na Shirika la World Vision Tanzania.

Alisema mpango huo unatoa nafuu kwa wananchi hivyo viongozi wote wa wilaya hiyo wanatakiwa kuhakikisha kwenye maeneo yao wananchi wanajiunga.

Emmanuel aliziomba taasisi na mashirika mengine kuiga mfano wa shirika hilo ambalo limekuwa sehemu kubwa ya kuisaidia serikali katika kutoa huduma mbalimbali za kimaendeleo hapa nchini.

"Ni muhimu mashirika na taasisi zilizopo kwenye wilaya hii kuhakikisha wanatoa huduma za kimaendeleo kama ilivyo kwa Shirika hilo la World Vision ambalo limekuwa msaada mkubwa kwa serikali katika sekta mbalimbali zikiwamo za kiafya, kielimu na nyinginezo," alisema.

Awali, Kaimu Mratibu wa Miradi wa World Vision Tanzania Wilaya ya Kongwa, Zacharia Shigukulu, alisema utoaji wa bima ni sehemu ya mpango kazi wa mwaka wa fedha 2021 katika juhudi zake za kuunga mkono serikali hasa kwa upande wa seka ya afya kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Alisema mpango huo unalenga kuwafikia wanufaika 1,800 ambao kati yao watoto ni 1,200 na watu wazima 600 ikiwa na lengo la kuchangia uboreshaji wa ustawi wa watoto familia zinazoishi katika mazingira magumu hadi kufikia 2025.

"Mpango huu umepitia mizunguko miwili ya miaka mitano na kila mmoja ukiachilia mbali miaka miwili ya kuanzia kwake, hivi sasa unatekeleza mkakati wake wa awamu ya tatu ya mwaka 2021- 2025 na bajeti ya Dola za Kimarekeni 400,000," alisema.

Shigukulu alisema shirika hilo limekuwapo nchini Tanzania takribani miaka 40 na linafanya kazi katika mikoa 14 ikiwamo Tanga, Kilimanjaro, Manyara, Arusha, Dodoma, Morogoro, Singida, Tabora, Simiyu, Shinyanga, Kagera, Kigoma, Dar es Salaam na Iringa kwa lengo la kuhudumia watoto milioni 4.5 kati yao waliosajiliwa 130,000.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Mkoka, Juma Budeba, alisema kwa kipindi cha Juni 2020 hadi Julai, mwaka huu, wamepata Sh. milioni 12.8 kutoka kwa wateja wa CHF.

Alisema kuwa kwa mwaka huu, wateja waliopo kwenye msamaha wa matibabu ya ni 7,585 sawa na Sh. milioni 46.9.

# Waziri ataka utafiti teknolojia ya ujenzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ameagiza Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) kufanya utafiti wa teknolojia ya ujenzi wa barabara za vijijini.

Ummy aliyasema hayo juzi alipokuwa akizindua kaulimbiu ya TARURA isemayo 'TARURA Tunakufungulia Barabara, Kufika Kusikofikika' katika kikao kazi cha siku tatu cha wakala na TAMISEMI, kinachoendelea jijini hapa.

"Nimearifiwa kuna kitengo cha utafiti TARURA. Nendeni mkafanye utafiti nimeambiwa kuna teknolojia ya kujenga barabara za vijijini. Badala ya lami, kuna teknolojia nyingine, nendeni mkafanye utafiti ili kujua teknolojia tutakayoitumia kwa ajili ya kujenga barabara za vijijini," alisema.

Aidha, alisisitiza usanifu wa madaraja ya bei nafuu vijijini ili kurahisisha usafiri kwa wananchi.

"Nimeona kulikuwa na mjadala wa lile daraja la Mlimba (lililogharimu Sh. milioni 31), lakini ukimsikiliza Mbunge wa Mlimba na wananchi lile daraja limekuwa mkombozi mkubwa kwao kwa kuwa watu walikuwa wanaliwa na mamba wakiwa wanavuka," alisema.

Ummy alisema hakuna haja ya kuwaza madaraja makubwa yanayohitaji fedha nyingi wakati inawezekana kupata daraja la gharama nafuu litakalosaidia wananchi kupita.

Pia Waziri Ummy alihimiza TARURA kutumia makandarasi walioko ndani ya mikoa husika na kutoa angalizo kwa wakala kuhakikisha kazi za ujenzi wa barabara zifanyike kwa ufanisi kwa kuwa ni kipimo chao kwa Watanzania.

"Tunataka tuone tija katika suala zima la ukarabati wa barabara mijini na vijijini, ndugu zangu mna kazi kubwa. Mwaka huu mmoja ndio mwaka wa kuwapima je, kile kisingizio cha kuwa hamna fedha kilikuwa kisingizio au hamna uwezo na ubunifu na utashi wa kazi mnazotakiwa kuzifanya?" Alisema.

Ummy alisema matarajio ya serikali kwa TARURA ni makubwa sana, hivyo wasiiangushe na waoneshe kuwa ni taasisi sahihi ya kufungua barabara za mijini na vijijini.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa TARURA, Mhandisi Victor Seff, alisema utekelezaji wa bajeti 2021/22 hadi Agosti 10, mwaka huu, mikataba 395 ya matengenezo ya barabara imetiwa saini na mingine 324 inatarajiwa kutiwa saini kabla ya Agosti 20.

Alisema kwa mwaka huo Wakala umeidhinishiwa bajeti ya Sh. bilioni 934.09 kutoka vyanzo mbalimbali ambapo kazi ya manunuzi itakamilika ifikapo mwishoni mwezi ujao.

"Katika kukabiliana na changamoto ya vitendea kazi, magari 100 na vifaa vya TEHAMA vitanunuliwa, kuajiri watumishi wa kada ya uhandisi 52, kuajiri wahandisi washauri watakaosimamia miradi mikubwa ya madaraja na barabara," alisema.



Mkuu wa Wilaya Bunda, Joshua Nassari (katikati), akikata utepe kuashiria kukabidhiwa rasmi kwa madawari 50 yaliyotolewa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB) kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Mariwanda A wilayani Bunda, mkoani Mara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana waonywa tamaa maisha ya mkato

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi, amewataka vijana kufanya kazi na kuacha tamaa ya kuwa na maisha mazuri kwa muda mfupi.

Katambi aliyasema hayo jana alipozungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Vijana Kimataifa iliyofanyika jijini hapa.

Aliwataka vijana nchini kufanya kazi ili kufanikiwa kimaisha na kuacha tabia ya kulalamika vijiweni na kutafuta maisha bora bila kufanya kazi.

"Tunajua ajira ni chache lakini kazi zipo nyingi unaweza kujiajiri mwenyewe kwa njia ya kilimo au kufanyabiashara hivyo tuondokane na malalamiko kuhusu ajira," alisema Katambi.

Alisema kazi ya serikali ni kuweka mazingira mazuri na watu wake ili kuzalisha uchumi na haiwezi kuajiri kila raia wake.

Aliongeza katika kuhakikisha vijana wanawezeshwa kiuchumi kupitia halmashauri kuna fungu limetengwa kwa ajili ya mikopo yao, lakini wanatakiwa kuunda vikundi.

Mwakilishi kutoka Shirika la Kimataifa la Tanzania Communications Analyst, Dk. Mariam Ngaenje, alisema takwimu zinaonyesha kwamba kuna vijana bilioni 1.2 wenye umri kati ya miaka 10 na 19 duniani kote kati ya hao milioni 207 sawa na asilimia 17.3 wanakabiliwa na tatizo la uzito uliokithiri.

Dk. Ngaenje alisema zaidi ya vijana bilioni 1.8 wenye umri kati ya miaka 15 na 24 wanaishi katika nchi zinazoendelea na nusu yao wanafanya kazi katika sekta za kilimo na chakula.

Alisema watoto wa kike wako katika hatari zaidi ya kupata utapiamlo kutokana na athari za mila na desturi ambazo husababisha ukosefu wa vyakula vyenye virutubisho, elimu bora na fursa za kiuchumi.

Dk. Ngaeje alisema kuwa UNFPA imedhamiria kusaidia vijana na taasisi zao kama ilivyobainishwa vizuri katika mkakati wa UNFPA wa vijana unaoitwa "My Body, My Life, My World".





# Malipo kadi chanjo corona kwa 20,000/-

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema serikali imeanza kutoa chanjo ya corona na imejiandaa kutoa vitambulisho kwa watu wote waliokamilisha chanjo ambayo gharama ya kadi hiyo ni Sh. 20,000.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wizarani kwake, Mnazi Mmoja, alisema kadi hiyo ni kielelezo ya kuthibitisha kuwa mtu amechanjwa na itasaidia hata kusafiri nje ya nchi.

Mazrui alisema ada hiyo ya kadi italipiwa kwa njia ya miamala ya kibenki na akaunti namba ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ambayo ni 0848946002.

"Kadi hii itapatikana hapa wizarani kitengo cha chanjo na lazima kwanza uchanje ndipo upatiwe kadi. Tumeamua kadi itolewe kwa malipo kwa sababu imetumika gharama katika utengenezaji," alisema.

Alisema watadhibiti utoaji wa kadi feki kwa sababu itatumika dunia nzima.

Pia alisema wametoa nafasi kwa waandishi wa habari kupata chanjo ya corona kuanzia Jumatatu ijayo kwa sababu watu wa kada hiyo ni kundi muhimu.

Alisema kwa sasa Zanzibar ina chanjo 85,000 elfu aina ya Sinivc kutoka China na Sphurtine ya Urusi ambazo hazina madhara na ukomo wake kumaliza muda ni mwaka mmoja.

Kwa mujibu wa waziri, chanjo zinazotolewa zinakubalika nchi nyingi duniani na baadhi ya nchi tu ndio hazikubaliani nazo ikiwamo Saudi Arabia.

"Nchi nyingi chanjo tunazotoa zinakubalika ni nchi chache tu ndio hazikubaliki lakini baadaye kutakuwa na chanjo nyingi ambapo wananchi watachagua wanazotaka," alisema na kuongeza kwamba zaidi ya watu 10,000 wamepatiwa chanjo na hakuna madhara yoyote yaliyotokea hadi sasa.

Hata hivyo aliwataka wananchi wote kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Serikali Mtandao, Said Seif Said, akizungumzia kuhusu ubora wa kadi za corona alisema rekodi za kiafya zitaonekana hadi mwenye kadi aingize nywila ya kadi hiyo.

Alisema taarifa za mtu atakayepewa kadi hiyo ambaye amechanja chanjo ya corona zitakuwa salama na zenye usiri mkubwa.




Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, akionyesha kadi maalum ya kielektroniki kwa waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, itakayotolewa kwa mtu atakayechanjwa chanjo ya corona, ambapo gharama yake ni 20,000/-. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SUZA, Huawei zaingia mkataba mafunzo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHUO Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kimetiliana saini hati ya ushirikiano na kampuni ya Huawei ili wanafunzi wa chuo hicho wanaosoma kompyuta na mawasiliano ya habari kupata huduma za kitaaluma.

Makubaliano hayo kwa upande wa Suza yamesainiwa na Kaimu Makamu mkuu wa chuo hicho Dk. Ali Makame na kwa upande wa Huawei yamesainiwa na mwakilishi wake Yohana Mathias yaliofanyika jana katika Chuo kikuu cha Suza huko Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja.

Mwakilishi wa Huawei, Yohana Mathias, alisema baada ya kutiliana saini makubaliano hayo kuwa kampuni hiyo ni ya kiteknolojia na inatambua umuhimu wa elimu na mchango wake katika kukuza maendeleo, hivyo wameamua kusaidia taasisi za elimu ya juu kwa lengo la kuwajengea uwezo wanafunzi.

Alisema kampuni hiyo inashirikiana na taasisi 18 za elimu ya juu kwa lengo la kuwajengea uwezo.

Mathias Alisema kwa Zanzibar ni SUZA pekee ndiyo yenye uhusiano huo, hivyo watashirikiana kuhakikisha vijana wanapata maarifa na ujuzi wa teknolojia za kisasa zinazotolewa na Huawei.

Alisema kampuni hiyo imekuwa na mashindano ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na SUZA imekuwa ikishiriki katika mashindano hayo na uhusiano na elimu ya juu umesaidia kuzalisha vijana wengi waliopata mafunzo kupitia kampuni hiyo na zaidi ya vijana 1,000 wameshanufaika.

"Huawei imejizatiti kutoa ushirikiano wa kutosha kwa taasisi ya elimu ya juu ili vijana kupata maarifa, ujuzi na uwezo unaohitajika katika soko la TEHAMA nchini," alisema.

Naye Ali Makame Ussi, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma, Utafiti na Ushauri), alisema makubaliano hayo lengo lake ni kupata huduma za kitaaluma ili kuwajengea uwezo wanafunzi wanaosoma fani za kompyuta na mawasiliano ya habari na kuwa na uelewa wa taaluma ya teknolojia.

Alisema Huawei ni moja ya kampuni kubwa zenye uzoefu mkubwa katika masuala ya kompyuta na teknolojia ya habari na kushirikiana nao inawapa nafasi ya kukuza ujuzi kupitia vijana na kushindana katika soko na kurahisisha uendeshaji wa maisha na kupata maendeleo kwa haraka.

# Maimamu wataka sababu kufungua tena kesi vileo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BODI ya Wadhamini wa Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) imeeleza sababu za kufungua kesi upya dhidi ya Bodi ya Vileo Zanzibar na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Imesema sababu kubwa ya kufanya hivyo ni baada ya kutoridhishwa na kufutwa kwa kesi ya awali na Jaji wa Mahakama Kuu, Rabia Hussein Muhammed.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari makao makuu ya JUMAZA, Majestic mjini Zanzibar, Katibu wa Kamati ya Maadili na Baraza la Taasisi za Kiislamu Zanzibar, Sheikh Abdallah Mnubi Abbas, alisema mahakama imekwepa kujibu hoja za msingi za kuvunjwa kwa Sheria ya Vileo Na. 9 ya mwaka 2020.

Sheikh Abbas alisema kwa mujibu wa kifungu 33(1) cha sheria hiyo, kampuni zinazotakiwa kupewa vibali vya kuingiza pombe mwisho ni tatu, lakini bodi imetoa kwa kampuni nane mpaka Februari, mwaka huu, kinyume cha sheria.

Alisema masharti ya sheria hiyo yameeleza anaepewa kibali lazima awe Mzanzibari, awe mlipa kodi, awe na ghala la kuhifadhia vileo na gari la kusambazia bidhaa hiyo.

"Kampuni zilizojitokeza baada ya kutangazwa zabuni zilikuwa tatu na ndizo zilizopitishwa, lakini badala yake kulianza kutolewa vibali vingine kinyemela kinyume cha sheria," alisema.

Pia alisema kifungu cha 28 (k) kinasema maduka ya kuuzia pombe na baa lazima yawe umbali wa mita 1,000 kutoka maeneo ya huduma za jamii kama hospitali, nyumba za ibada, madrasa na makazi ya watu, lakini bodi imeshindwa kusimamia masharti hayo.

Alisema inasikitisha mpaka sasa Bodi ya Vileo haijachukuliwa hatua yoyote tangu kuanza kuvunjwa kwa sheria licha ya viongozi kula kiapo cha kulinda katiba na sheria katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kabla ya sheria kutungwa, alisema ilipitishwa katika vikao vizito vya serikali kuanzia makatibu wakuu, baraza la mawaziri na kuwasilishwa mswaada wa Sheria ya Baraza la Wawakilishi na kuanza kutumika baada ya kutiwa saini na aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein.

Alisema wakati serikali inaendelea kukabiliana na tatizo la udhalilishaji wa wanawake na watoto, lakini imeshindwa kuangalia chimbuko la kuongezeka kwa vitendo hivyo ikiwamo uingizaji holela wa pombe kutokana na sheria kutokusimamiwa.

Jaji Rabia alifuta kesi iliyofunguliwa na JUMAZA kwa madai ya kufunguliwa kinyume cha sheria baada ya kuishtaki Bodi ya Vileo badala ya mwanasheria mkuu wa serikali na kushindwa kutoa idhini ya kuishtaki serikali kwa muda wa siku 60 kabla ya kufungua kesi.



**RICH OGANURU AKUMBUKWA KWA MENGI**

Ukurasa14

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI AGOSTI 14, 2021



## MASKINI MUNA LOVE

# Afurahia 'dimpozi', lakini kuna madhara

UPASUAJI wa kurekebisha viungo unaonekana kuongezeka miongoni mwa mastaa hapa nchini, katika tukio la hivi karibuni Mwigizaji Muna Love, alitangaza kuchukua mkondo huo kwa kutengeneza mashavu yake.

Muna Love, aliweka wazi kwamba amefanya upasuaji wa kuweka 'dimpozi' kwenye mashavu yake na kuelezea ilikuwa ndoto yake ya siku nyingi.

Katika kuonyesha kwamba hiyo si mara yake ya kwanza, msanii huyo amesema amerekebisha viungo vyake mara nne na bado ataendelea kufanya hivyo hadi atakapoona inatosha.

Kuna wasanii wengine wamefanya upasuaji wa aina hiyo licha yao wenyewe kukanusha mara kadhaa, Wema Sepetu, anadaiwa kufanyiwa upasuaji wa aina hiyo mara kadhaa.

Baadhi ya mashabiki wa Muna Love, wamekuwa na maoni tofauti, kuna wale waliompongeza na wanaopinga wakisema upasuaji huo unakwenda kinyume na matakwa ya Mungu.

Kulingana na tafiti mbalimbali, upasuaji wa kurekebisha viungo una madhara mengi kuliko faida. Wanasema baadhi ya madhara hayo ni kupata maambukizi kwenye damu, saratani na mwili kupata mzio.

Utafiti uliotolewa na BBC, umenukuu baadhi ya madaktari wakiwashauri watu wanaotaka kufanya upasuaji kupata muda wa kufikiria, pia kuacha tabia ya kukimbilia hospitali zisizo na huduma za kutosha ambazo zinatoza gharama nafuu katika operesheni za aina hiyo.

Ripoti ya Deloitte, inaeleza soko kubwa na kubadilisha viungo lipo China, na wasanii wengi wanakwenda huko kutokana na gharama zake kuwa nafuu.

Watu wengi wanajali kuwa warembo, lakini hawaangalii athari za baadae baada ya upasuaji, jambo ambalo linaleta wasiwasi kama wataweza kumudu gharama ya kutibu na dalili za athari hizo.

BASI SAWA

## Wagosi wa Kaya jitokezeni



NANI kasema kundi la Wagosi wa Kaya limekufa? Kama watu wenye mawazo hayo, basi watakuwa na ndoto za mchana, kwani wao wenyewe wamesema  bado wapo sana tu.

Mmoja wa waimbaji wa kundi hilo, Mkoloni amesema Wagosi wa Kaya wanaendelea kuchapa kazi na kama watafikiria kufanya hivyo, itakuwa wamekataa muunganiko wao na jamii.

"Ni muda mrefu tumekaa nje ya game lakini Wagosi wa Kaya hatuwezi kuacha muziki kwa sababu umetuunganisha na jamii,  ina maana tukiacha itakuwa tunakataa muunganiko wetu na jamii kitu ambacho hakiwezekani" amesema Mkoloni.


## Bob Junior kama hivyo hujafulia



MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Bob Jonior, ameibuka baada ya kupotea kwa muda mrefu, akisema yeye bila shilingi milioni moja, hawezi kwenda matembezini.

Bob Junior, ambaye miaka ya nyuma alitamba kimuziki, amesema kiasi hicho cha pesa anakitumia kwa masaa kadhaa tu, kwani huwa anaambatana na kundi la wasaidizi wake.

"Mimi nina 'team' ya watu wengi, nikitoka lazima niwe na milioni moja tu, halafu milioni moja si pesa ya kawaida tu" ameiambia EATV alipoulizwa kiasi gani anatumia akiwa matembezini.



## Baba Levo mwache akayaone hukohuko

MWANAMUZIKI na mchekeshaji, Baba Levo, amemtaka msanii mwenzake Rayvanny, kufikiria mara mbili kabla ya kuamua kuoa.

Hivi karibuni, Rayvanny kupitia Insta Story,aliandika jinsi alivyoshindwa kusubiri hasa suala la ndoa yake.

Baba Levo, aliibuka na kumshauri asiwe na haraka kwa sababu hakuna anachokimbilia na anatakiwa kutuliza akili zake kwanza.





## Mose Iyobo mapenzi yanamtesa

KWELI mapenzi upofu! Ndivyo inavyoonekana kwa mnenguaji kutoka WCB, Mose Iyobo, baada ya kumtaja Ruby kama faraja yake baada ya kukumbana na vikwazo vingi.

Bila kumtaja jina, Iyobo amesema mwanamke aliyekuwa naye sawa na shetani, hivyo akamsihi Ruby, kutokwenda kwa mganga wakati bado wana nguvu.

"Shetani aliniwekea vikwazo vingi ila sasa kashindwa, Sali na  usiende kwa mganga tunguli huisha nguvu" – ameandika Iyobo katika akaunti yake ya Instagram.

## Hawa huwezi kuwafikia kirahisi

**Na Adam Fungamwango**

ZAMANI tulikuwa tunaona kwa wenzetu nje ya nchi wasanii wakubwa wakitembea na walinzi.

Nchini Tanzania miaka ya nyuma haikuwa hivyo. Lakini miaka inabadilika na maisha yanabadilika.

Kwa sasa nchini kuna baadhi ya wasanii wamekuwa wakilindwa mithili ya viongozi. Kuna baadhi ya wasanii wakishapata majina makubwa tu, utaona wanaanza kutembea na mabaunsa au walinzi wao binafsi.

Tabia hii kwa sasa imekuwa kubwa sana Bongo hasa kwa baadhi ya wasanii wanoona wamefika viwango fulani vya umaarufu, hivyo kuhitaji 'mabodigadi'.

Kwa baadhi ya watu imeonekana kuwa ni gumzo, vituko, vichekesho, majisifu, majigambo, usumbufu kwani wanaona hala hakuna umuhimu wa hilo.

Wengine wanafanya kwa fasheni tu kwa sababu mtu fulani ana walinzi.

Ukweli ni kwamba kwa sasa nchini kuna baadhi ya wasanii ambao wamekuwa vipenzi vya mashabiki na umaarufu wao unawalazimisha kuwa na walinzi ili kumuepusha na hatari yoyote inayoweza kutokea kwenye safari zake za kibinafsi, kifamilia, misele yake ya kila siku, studio, kupiga picha za video au kutambulisha ngoma.

Leo tutawaangalia wasanii wa Kibongo ambao kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali, ndiyo wanaoongoza kwa kulindwa au kwa ulinzi mkali kuliko wengine.

**5. NANDY**

Jina lake kamili ni Faustina Charles. Jina lake maarufu la kimuziki ni Nandy. Anatembea na 'mabodigadi' wawili ambao huambatana naye kila anakopita. Akienda kushuti video, kununua nguo au bidhaa, au kutambulisha ngoma ni lazima aambatane na mibaba hiyo iliyoshiba, yenye uwezo wa kufanya chochote inapoona bosi wao yupo kwenye hatari.

**4. ZUCHU**

Kwa sasa hakuna mtu anayehoji uwezo wa msanii huyo wa kike ambaye ameibuka kwa kasi na kuwa staa kamili. Na hata umaarufu wake umekuwa wa juu sana kiasi sasa naye kuhitaji walinzi.

Anatembea na walinzi wawili waliotuna. Huwezi kumsogelea kwa karibu hadi upate ruhusa maalum.

**3. RAYVANNY**

Huyu pia ni mmoja wa wasanii wanaoongoza kuwa na ulinzi mkali. Ila tofauti ni kwamba mabaunsa waomlinda Rayvanny wao hawavai suti. Kama kuanza waanze leo.

Wao wanavaa nguo za kawaida zozote zile wanazoona zinavaa kwa siku hizo au kwa sababu maalum.

**2. HARMONIZE**

Konde Boy yeye anatembea na 'mabodigadi' kama wanne hivi. Lakini mara nyingi sana wanakuwa watatu. Nadhani mmoja anakuwa amebaki kulinda nyumbani wakati mwingine. Mabaunsa wake mara zote wanaonekana kuwa makini mno. Huyu alianza kuwa na walinzi pale tu walipojiunga na WCB.

**1. DIAMOND PLATINUMZ**

Huyu ndiye baba lao. Si kwenye muziki tu, bali hata kwenye ulinzi. Ana walinzi au 'mabodigadi' kila sehemu anapokanyaga. Analindwa kwa gharama kubwa kwa sababu kwa sasa ndiyo kioo kwa Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Mara nyingi anakuwa na walinzi wanne. Diamond ndiye msanii mwanzilishi wa kuwa na mabaunsa nchini.






## Siri ya Marehemu; Chaguliwa na watu, si mizimu

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA uongozi wowote ule duniani, inatakiwa upendwe na watu. Ni kwa sababu kiongozi yoyote yule huongoza watu na si vinginevyo. Kiongozi wanayeutafuta uongozi kwa nguvu, au kwa hila yoyote ile ni hatari sana. Kwa sababu anaweza kufanya lolote lile ili tu achaguliwe au endelee kukaa madarakani hata kama watu hawataki.

Filamu au 'Siri ya Marehemu' ina kisa ambacho ni fundisho kwa baadhi ya watu ambao badala ya kueleza sera kwa wananchi na kuwashawishi, au wanaenda kinyume na kufanya ushirikina ili washinde.

Imechezwa na Joseph Otieno, Issa Rioba, Mohamed Fungafunga, Sharifu Kumwenda na wengineo.

Kwenye kijiji kimoja cha Mbwawa Mkoleni, anaonekana mwanakijijii mmoja anampigia hodi mjumbe huku akipiga kelele kana kwamba nje kuna kitu cha hatari. Mjumbe ambaye ni mzee Jengua anamfungulia. Lakini baada ya muda anatoka na kuonekana hataki kulala kwa mjumbe. Lakini kabla ya kuondoka kuna kitu anamwambia.

Mwanakijiji huyo ni Kilindo. Lakini tangu aagane na mjumbe wa kijiji, hajaonekana tena na siku ya nne akaonekana na amefariki nyumbani kwake.

Mjumbe anakusanya baadhi ya watu na kuwaambia kuwa mara ya mwisho waliopoagana alipoondoka kwake alikwambia maneno yafuatayo.

"Kijiji hiki msipoangalia mtaangamia.Kuna mambo makubwa yatatokea." Mzee Jengua akasema kuwa alimuuliza marehemu ni kitu gani, akamwambia atamwambia kesho, Baada ya hapo hakuonekana kwa siku nne, badala yake ikaonekana maiti yake tu.

Baada siku kadhaa mzee Jengua akaenda kwa Mwenyekiti kumuambia uwezekano na kuchunguza kifo cha Kilindo, lakini naye anafariki ghafla akiwa ofisini.

Wakati mambo hayo yote yanatokea kilikuwa ni kipindi cha uchaguzi, na Mwenyekiti Baba Kibwana, alikuwa kwenye harakati ya kufanya kampeni ili ilichaguliwe kwa muhula la pili.

Kifo hiki cha Jengua kinaleta mtafaruku kwenye familia hizi mbili kiasi kwamba ziliwagawa wanakijiji pande mbili. Wengine walimtetea Mwenyekiti ambao ndiyo walikuwa wengi zaidi na wachache waliitetea familia ya Jengua ambayo ilikuwa imechachamaa kwa kumwita Mwenyekiti ni mchawi. Na sasa akavumishwa kubwa ndiye aliyemuua Kilindo na Jengua pia.

La mgambo litaitwa kijijini ili wanakijiji wote kwenda kwenye mizimu kuuliza kulikoni matukio yanayotokea hapo kiasi kwamba watu hawaelewani.

# BBNaija yazidi kunoga



SHINDANO la Big Brother Nigeria (BBNaija) linazidi kunoga, baada ya washiriki watatu kuondolewa ndani ya nyumba na kuingizwa wengine wanne

Walioaga shindano hilo siku ya Jumapili iliyopita ni Arin, Nini na Princess.

Hata hivyo, washiriki walishtuka baada ya Big brother kutangaza ujio wa washiriki wapya ambao waliingia kwa mbwembwe ndani ya jumba hilo.



## Rich Oganuru akumbukwa kwa mengi

WANIGERIA na wapenzi wa filamu za Nollywood, wanazidi kuomboleza kifo cha mkongwe Rich Oganiru, ambaye alifariki wiki hii.

Msanii huyo mwenye kipaji cha hali ya juu cha uigizaji, alifariki siku ya Jumanne baada ya kuugua kwa miezi kadhaa.

Taarifa ya kifo chake kilitolewa na rafiki yaje EmstarVee, akimuelezea kuwa alikuwa rafiki mwema kama kaka yake.

Wiki mbili zilizopita ilisambaa video fupi katika mitandao ya kijamii ikimuonyesha Oganiru, amelala kitandani akiumwa.

## Tonto aamua kurudi darasani

MWIGIZAJI kutoka Nollywood,Tonto Dikeh, ameamua kurudi tena darasani kwa ajili ya kuongeza elimu yake.

Kupitia akaunti yake ya Instagram, Tonto, ameweka picha tofauti zikimuonyesha akiwa ndani ya darasa la chuo kimoja nchini humo.

Msanii huyo aliyefanikiwa kukusanya tuzo mbalimbali, amejiunga katika chuo cha utunzaji wa mazingira na kuwataka mashabiki wake kumuombea apate mafanikio katika safari yake hiyo ya elimu.





## Beyonce ajivunia figa

STAA wa muziki wa Marekani, Beyonce, ameweka wazi kwamba umbo lake jipya linatokana na mapambano yake kufuata utaratibu wa lishe.

Akizungumza na jarida la Harpers Bazaar, mwanamuziki huyo amesema wakati mwingine hakupata usingizi wa kutosha kutokana na mpangilio wa chakula katika maisha yake yote ya kisanii.

"Binafsi nimejitahidi kupambana na tatizo la kukosa usingizi zaidi ya nusu ya maisha yangu. Miaka ya kuvaa na kuimarisha misuli yangu kutokana na kucheza kwa visigino," amesema Beyonce.

## Mke wa Eminem nusura ajiue

ALIYEKUWA mke wa rapa maarufu wa Eminem, amelazwa hospitalini baada ya kujaribu kujiua.

Kulingana na TMZ, polisi na wafanyakazi wa dharura walipigiwa simu Julai 30, mwaka huu na mtu wakifahamishwa katika nyumba Kim Scott huko Michigan, kuna mtu anajiua.

"Kim alikuwa akipiga watu, ilibidi azuiliwe na wasaidizi na alikuwa mkali. Wahudumu wa afya hawakuweza kuangalia tukio hilo," ilisema ripoti hiyo.

"Kim alikuwa amejikata, alikuwa na maumivu mengi na nyuma ya mguu wake kulikuwa na damu nyingi zikimwagika sakafuni,"

Scott na Eminem walifunga ndoa mwaka 1999 na waliachana mwaka 2001.



MAKALA

# DIT inapojikita kuonyesha fursa katika soko la TEHAMA viwandani

**Na Sabato Kasika**

TAIFA linapokuwa na vijana wenye elimu, ni rahisi kupata maendeleo ya haraka kutokana na kuanzishwa viwanda, ongezeko kubwa la ajira na ufanisi wa kazi.

Kinachozingatiwa ni upatikanaji wa ubora wa fani mbalimbali katika maeneo ya kazi kulingana na mabadiliko ya haraka yanayojitokeza katika nyanja hizo, hasa elimu ya ufundi.

Elimu ya ufundi, inatajwa kuwa ni muhimu kwa kuwajengea vijana stadi za kazi na inaweza kuwasaidia kupata ajira haraka kama fani walizosoma zimejikita kwenye matarajio ya waajiri.

Kwa kutambua umuhimu huo, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), imelitoa mafunzo kwa wanafunzi wake yenye lengo la kuwaandaa kuingia katika soko la ajira watakapohitimu masomo yao chuoni hapo.

Mratibu Msaidizi wa mradi wa mafunzo hayo uitwao East Africa Skills Transformations for Regional Intergration Project (EASTRIP), kutoka taasisi hiyo, Daud Mboma, anaelezea zaidi mafunzo hayo yataongeza uwezo kwa vijana ili kutambua umuhimu wao katika kazi pale watakapoajiriwa au kujiajiri.

"Tunatarajia kwamba, asilimia 50 ya vijana watakaohitimu chuoni hapa ndani ya meizi sita watakuwa wamejiajiri au kuajiriwa katika elimu ya TEHAMA watakayokuwa wameipata," anasema Mboma.

Mratibu huyo anasema, mafunzo hayo yatakuwa endelevu hadi mwaka 2024, na kwamba yatawanufaisha vijana wengi kutoka chuoni hapo.

"Tunakusudia kuboresha elimu ya ufundi katika eneo la TEHAMA hasa kuhusu utaalamu wa mitambo ya viwandani na kuendeleza weledi kwa wanafunzi katika soko la ajira ambalo sasa lina ushindani mkubwa," anasema Mboma.



Mkufunzi Daud Mbona (aliyesimama) akitoa mafunzo kwa wanafunzi wa chuo hicho wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Anaeleza, DIT imefanikiwa kuboresha mitaala katika masomo yake ili kwenda sambamba na mahitaji ya soko hasa viwanda.

Katika mkakati huo, wanafunzi na walimu wamepata nafasi kutembelea viwanda mbalimbali ili kuona teknolojia inavyofanya kazi.



Jinsi TEHAMA inavyofanya kazi. **PICHA: MTANDAO**

"Unajua mitambo mingi kwenye viwanda ni ya kisasa ambayo ni muhimu kuielewa, hivyo nasi tumeona kuna haja ya kuzingatia hilo kwa kuangalia mahitaji ya viwanda husika," anasema.

Mratibu huyo anasema, aina za kazi kwenye viwanda nimewafanya kuona fursa ya kuwaandaa wanafunzi kwa ajili ya kukabiliana na hali ya soko.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo kutoka Taasisi ya Civil People of Tanzania, Makei Moshi, anasema, mbali na mambo ya mitambo ya viwandani, bado baadhi ya vijana wanahitaji kupata elimu zaidi utambuzi.

"Vijana wengi bado wana tatizo katika uchanganuzi wa masuala kama utambuzi binafsi kwenye matumizi ya mitandao ya kijamii na uandishi wa wasifu," anasema Moshi.

Anasema, si hapo tu mambo mengine yanayohusiana na mifumo ya TEHAMA katika masoko ya ajira bado wako nyuma, wanahitaji kusaidiwa zaidi kuingia katika soko la ajira.

"Vijana wanaohitimu vyuo ni wengi, lakini ugunduzi wa matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii bado ni tatizo kwao, kwa kuwa mafunzo haya ni endelevu hadi mwaka 2024, ninaamini matatizo katika eneo hilo yatapungua," anaongeza kusema.

Mwanafunzi aliyeshiriki mafunzo hayo, Sozi Abdul, anakiri uwepo wa tatizo hilo na kusema kabla ya mafunzo alikuwa hajui matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii katika kutafuta kazi.

"Baadhi ya vijana na watu wengine wanashinda kwenye mitandao ya kijamii kwa mambo ambayo si ya msingi, lakini kwa elimu hii nimejua vitu vingi ambavyo nitafanyia kazi," anasema Abdul.

Anasema, kwenye mitandao ya kijamii hasa simu na kompyuta, mwanafunzi anatakiwa kuitumia kwa mambo ya msingi yanayohusu masomo kwa manufaa ya muhusika na jamii kwa ujumla.

# SEIF AL ISLAM APATA KIKWAZO

## ●Ni mtoto wa Gaddafi aliyetaka kuwania urais
## ●Hati ya kukamatwa yatolewa akikanyaga Libya



Na Mwandishi Wetu

WAENDESHA mashtaka nchini Libya wametoa waranti ya kukamatwa kwa Saif al-Islam Gaddafi, ambaye ni mtoto wa aliyekuwa kiongozi wa Libya marehemu Muammar Gaddafi, akituhumiwa kuwa nyuma ya mamluki wa Urusi.

Hati hiyo ya kukamatwa itafifisha ndoto yake ya kurudi nchini humo ili kuwania kiti cha urais ambacho baba yake alikuwa nacho miaka 10 i liyopita.

Uchunguzi uliofanywa na BBC, umebaini kundi la Wagner, lilifanya vitendo vya kihalifu dhidi ya raia wa nchi hiyo na kuleta madhara mengi.

Wapiganaji wa Urusi ambao wanahusishwa na kundi hilo, walionekana kwa mara ya kwanza nchini Libya mnamo mwaka 2019 walipojiunga kusaidia vikosi vya mbabe wa kivita jenerali, Khalifa Haftar.

Mamluki hao na waasi walikuwa wakiishambulia serikali inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa katika mji mkuu Tripoli.

Mzozo huo ulimalizika kwa makubaliano ya kusitisha mapigano Oktoba, mwaka 2020.

Kikundi cha Wagner kiligunduliwa kwa mara ya kwanza mwaka 2014 wakati kilikuwa kikiunga mkono wapiganaji wanaotaka kujitenga wanaoungwa mkono na Urusi katika mzozo mashariki mwa Ukraine.

Tangu wakati huo, kundi hilo limehusika katika mizozo ya Syria, Msumbiji, Sudan na Jamhuri ya Afrika ya Kati.

Amri ya kukamatwa kwa Saif al-Islam Gaddafi, imesambazwa Agosti 5, mwaka huu katika vyombo vya usalama vya Libya na mwendesha mashtaka, Mohammed Gharouda.

**KUSHUKIWA KWA SEIF AL-ISLAM**

Kwa muda mrefu Gaddafi alishukiwa kuwa na uhusiano na Urusi.

Kabla ya ghasia za mwaka 2011, aliaminiwa na wengine kama mtu anayependa mageuzi ya taratibu nchini Libya, wakati huo Muammar alikuwa kiongozi wa nchi hiyo.

Seif ni mzungumzaji mzuri wa Kiingereza ambaye alisoma katika Shule ya kifahari ya London school of Economics, kwa muda mrefu alionekana kama mmoja wa watu wenye ushawishi mkubwa nchini humo, na mrithi wa baba yake.

Hata hivyo, sifa hiyo ilipotea wakati wa maandamano dhidi ya serikali ya baba take yalipoanza, mwaka 2011, alijiunga na msako dhidi ya waandamanaji waliopinga serikali ya baba yake.

Baadhi ya wanafamilia yake mwishowe waliuawa au kukimbia nchi. Seif alikamatwa na waasi mwishoni mwa mwaka 2011 na kupelekwa katika mji wa Zintan, ulioko kusini magharibi mwa Tripoli. Huko aliachiliwa na wanamgambo waliomshikilia kwa miaka sita.

Wakati akiwa kizuizini, alihukumiwa kifo akiwa hayupo na mahakamani kwa kuhusika na mauaji ya waandamanaji.

Anatafutwa pia na Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) kwa uhalifu dhidi ya binadamu uliofanywa wakati wa ukandamizaji.

Ingawa hajaonekana hadharani kwa miaka mingi, Seif Al-Islam alifanya mahojiano na gazeti la New York Times, mwezi uliopita na akazungumzia mipango yake ya kurudi kwenye siasa.

Wakati wa utengenezaji wa makala ya BBC juu ya shughuli za kikundi cha Wagner huko Libya, BBC ilikutana na maofisa wa ujasusi wa Libya ambao walizungumza juu ya uhusiano mkubwa kati ya Seif na Urusi.

Maofisa wa ujasusi walikuwa wakimchunguza Maxim Shugaley, raia wa Urusi ambaye alikamatwa mjini Tripoli mwezi Mei mwaka, 2019 kwa mashtaka ya ujasusi.

Alishutumiwa kwa kumfanyia kazi Yevgeny Prigozhin, mfanyabiashara tajiri aliye na uhusiano wa karibu na Rais Vladimir Putin, kama sehemu ya kampeni ya kuingilia uchaguzi iliyoundwa kumweka Gaddafi kama mtawala wa Libya wakati wa mashambulizi ya Jenerali Haftar dhidi ya mji mkuu.

Shugaley na mkalimani wake wa Kiarabu ambaye alikamatwa pamoja naye, waliachiliwa mwishoni mwa mwaka 2020.

Kulingana na ripoti hiyo, Shugaley alikuwa amekutana na mtoto huyo wa Gaddafi wakati alipokuwa Libya.

Urusi imetoa filamu mbili juu ya kukamatwa kwa Shugaley, ambazo zimechapishwa kwenye mtandao wa YouTube na zinaonyesha Seif kama mwokozi wa Libya na Shugaley kama shujaa wa Urusi.

Utawala Kanali Muammar Gaddafi, wa zaidi ya miongo minne uliishia katika ghasia baada ya mapinduzi ya Kiarabu. Alijaribu kukimbia lakini akakamatwa na kuuawa.



## China yakataa WHO uchunguzi mpya chimbuko la virusi corona

**Hongkong,** CHINA

CHINA imeukataa wito wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusu kufanyika uchunguzi mpya juu ya chimbuko la virusi vya corona, ikisema inaunga mkono juhudi za kisayansi badala ya kisiasa ili kubaini chanzo cha virusi hivyo.

Shinikizo linazidi kuongezeka kwa China kufikiria kufanyika upya uchunguzi juu ya uliokoanzia ugonjwa wa Covid-19 uliosababisha vifo vya zaidi ya watu milioni nne na kuathiri uchumi wa dunia, tangu ugonjwa huo uliporipotiwa kwa mara ya kwanza katika mji wa Wuhan.

Juzi, WHO liliihimiza China kutoa takwimu ilizonazo kufuatia maambukizo ya kwanza ya virusi vya corona ili kuchunguza chimbuko la ugonjwa huo.

China ilijibu kwa kusisitiza msimamo wake kuwa uchunguzi wa awali juu ya chimbuko la virusi hivyo unatosha, na kwamba wito wa kuitaka China kutoa data zaidi juu ya ugonjwa huo unashinikizwa kisiasa.

**DW**

## Kura zahesabiwa Zambia uchaguzi mkuu wa rais

**Lusaka,** ZAMBIA

TUME ya uchaguzi ya Zambia, jana ilianza kutangaza matokeo ya uchaguzi wa urais ambao umegubikwa na kuzuiwa kwa mtandao wa Intaneti na kuripotiwa machafuko katika mikoa mitatu nchini humo.

Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zambia ECZ Patrick Nshindano, aliesema tume hiyo itaanza kutangaza matokeo hayo kuanzia saa nne asubuhi.

Tume hiyo ilisema matokeo kamili ya uchaguzi huo yatajulikana siku tatu tangu vituo vya kupigia kura kufungwa.

Miraim Makonda, ofisa msimamizi katika kituo cha kupigia kura alisema, "Leo imekuwa nzuri. Tumefanya kazi nzuri sana na hatukuwa na matukio yoyote mabaya. Ndio, zoezi linaendelea vizuri.

Hata hivyo, serikali imekataa kuzungumzia juu ya kukatika kwa mtandao wa Intaneti, baada ya watumiaji wa mtandao kusema walishindwa kutumia mitandao yao ya kijamii.

Mamilioni ya Wazambia walijitokeza juzi Alhamisi kupiga kura na kulazimisha baadhi ya vituo vya kupigia kura kubaki wazi kwa saa nyingi.

**DW**

# Mtanzania Maryam Salim ateuliwa meneja Benki ya Dunia Cambodia

**Washington,** MAREKANI

BENKI ya Dunia (WB), imemteua Mtanzania Maryam Salim kuwa meneja mpya Cambodia.

Maryam amekuwa mrithi wa Inguna Dobraja, ambaye amehamia Moldova baada ya miaka mitano ya kuwa Mkuu wa ofisi ya Benki ya Dunia (WB), Phnom Penh.

Amefanya kazi benki hiyo kwa zaidi ya miaka 20, hivi karibuni alikuwa meneja wa Albania.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa, Maryam atafanya kazi za kila siku za benki hiyo akishirikiana na serikali na washirika wa maendeleo, ikiwamo miradi ya thamani ya dola bilioni 1.1.

Miradi hiyo imeunganishwa na vipaumbele vya maendeleo vya Cambodia na malengo pacha ya WB, kupunguza umasikini na kuongeza ustawi wa pamoja.

"Ni furaha yangu kuchukua msimamo huu mpya na ninafurahi sana kurudi Cambodia, miaka 17 baada ya kufanya kazi hapa kama kiongozi wa timu ya miradi ya mifuko ya kijamii kuimarisha jamii na kupambana na umaskini," alisema Maryam.

"Ninatarajia kufanya kazi na wenzangu wa Cambodia kusaidia nchi kudhibiti athari zinazoendelea za janga la Covid-19, kujenga ujasiri dhidi ya mshtuko wa kiuchumi wa siku zijazo."

Maryam si mgeni Cambodia, amewahi kufanya kazi kama mtaalam wa maendeleo ya kijamii huko na ameshikilia nyadhifa kadhaa za juu katika sera ya shughuli za benki, Washington D.C.

Ana shahada ya uzamili ya uchumi wa Kimataifa na Uhusiano kutoka Chuo Kikuu cha Johns Hopkins na shahada ya Uzamivu ya Falsafa ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Georgetown. **BBC**



Moshi ukiwa umesambaa katika Jiji la Kandahar, Kusini Magharibi mwa Afghanistan, baada ya mapigano ya vikosi vya serikali na Taliban, juzi. **PICHA: AP**

# Taliban waumiliki mji wa Kandahar

**Kabul,** AFGHANSTAN

WANAMGAMBO wa Taliban wamechukuwa udhibiti wa mji mkuu wa jimbo la Kusini la Kandahar, huku Marekani na Uingereza zikituma ndege za kuwahamisha raia wao kutoka Afghanistan.

Ujumbe kupitia Twitter uliotumwa na msemaji wa Taliban siku ya jana, ulisema: "Kandahar yote imekombolewa. Wapiganaji wa jihadi wamefikia Uwanja wa Mashujaa."

Madai hayo yalithibitishwa pia na mkazi mmoja aliyeliambia shirika la habari la AFP kwamba, vikosi vyote vya serikali vilikuwa vimekimbilia kwenye kambi moja ya kijeshi iliyo kusini mwa mji huo.

Wabunge wawili, Gul Ahmad Kamin na Arif Noorzai, waliliambia shirika la habari la Ujerumani (dpa) kwamba kabla ya kuweka silaha chini na kukimbia, vikosi vya serikali vilipambana dhidi ya wanamgambo wa Taliban kwa zaidi ya wiki mbili.

Baada ya kufanikiwa kuuchukua mji huo wenye wakazi wapatao 651,000 na ambao ni wa pili kwa ukubwa Afghanistan baada ya mji mkuu Kabul, sasa wanamgambo wa Taliban wanadhibiti miji mikuu 13 ya majimbo kati ya majimbo 34 ya Afghanistan

**DW**

# Idadi wazungu Marekani yashuka kwa kasi kipindi muongo mmoja

**Washington,** MAREKANI

INASEMEKANA idadi kubwa ya watu wenye rangi tofauti inaongezeka wakati idadi ya wazungu ikiwa imepungua katika mwongo mmoja uliopita.

Hilo limejitokeza kwa mara ya kwanza katika historia ya Marekani kupitia sensa mpya ya iliyofanyika mwaka jana.

Idara ya sensa juzi ilisema hesabu yake ilionyesha kwamba kulikuwa watu millioni 331.4 wanaoishi Marekani, likiwa ongezeko la asilimia 7.4 tangu mwaka wa 2010.

Lakini taswira ya taifa kulingana na rangi na kabila ilibadilika, watu wamekuwa wakihamia mara kwa mara kwenye miji mikuu, mara nyingi kwenye majimbo ya Kusini na Magharibi, na Wamarekani ambao wamekuwa mara nyingi wakiondoka kwenye jamii ndogo, mwishowe idadi yao ilipungua.

Watu wanaotambulika kama wazungu bado ni kundi kubwa la raia wa Marekani, idadi yao ilipungua kwa asilimia 8.6 kuliko mwaka wa 2010.

Kundi kubwa la kufuata la watu wanaotambulika kama wa Hispanic Walatino, walikuwa sawa na milioni 62.1 mwaka wa 2020, likiwa kundi la wa Marekani ambalo liliongezeka kwa asilimia 23 katika muongo mmoja.

Wamarekani weusi walikuwa takriban milioni 46.9, huku Wamarekani wenye asili ya Asia wakiwa takriban milioni 24.

**VOA**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**LOREEN PRIMI MUSHI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0692/0026** kilichototlewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **ROSMINI** mwaka **2018,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/MSI/RB/396589/2021**

116406802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo MKURANGA**
**WILAYA YA MKURANGA**
**Usimamizi wa mirathi**
**Na,49/2021**

Ombi la **DAUDI MLOGE SHAYO** kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **JAMILA ABDULLAHAMID NZOTA**

Kwa **YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi mnamo **tarehe 16/08/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

Kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa

116406902

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**DONALD MAJANJARA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S353/0021** kilichotolewa na baraza ka mitihani kupitia shule ya secondary ya **PARANE** mwaka **1997**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/MAG/RB/397922/2021**

116407002

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.244/2021**

Ombi la **NIXON JULIUS MTATIFIKOLO** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **PAULO MATHEW MTATIFIKOLO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 16/08/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 12/08/2021**

116407502

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **FREDY PETER KITWANGE** anatangaza kupotelewa kwa kadi yake ya pikipiki(Haujue) aliyouziwa na kampuni ya **GS GROUP LIMITED** yenye usajili Namba. **MC 222 CNZ** Chasis Namba. **LC6PCJK23L0009494** Engine Namba.**156FM15AD2F75464** Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Rb Namba.**MOR/MOR/RB/386049/2021.**

116407602

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 29/ 2021**
**In the matter of the Estate of the late JOHN EMILIAN PUKULE of Nkuhungu Area within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTATION BY JANETH ISDORI MWINGIRA**
**AND**
**ABDONI HERMAN**
**GENERAL CITATION**
***(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 163)***

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or **before 20 Day of 8/2021.**
**Date at Dodoma this 24TH Day of May 2021**

RESIDENT MAGISTRATE

116408002

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 74 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE CHARLES BENJAMINI ULANGA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY MARY MVUNGI**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations IS made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the ……. Day of……….2021.
Dated at Dodoma this 6th day of August 2021

…………………………………………
**PETITIONER**
Presented for filling this 11th day of August 2021

…………………………………………
**MAGISTRSTE**

116408102

---

## KUOTEA KWA KADI YA GARI

**CLEMENCE SIMON WIHOMBE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI CANTER** yenye namba za usajili **T 102 DJR**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **NJ/TR/RB/402/2021**

116408202

---

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.

Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake imekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.

Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka mke wangu-7

Mtunzi anapatikana (0716 350534)

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI anaoga, ilikuwa ni fursa kwake sasa kurejea kwenye hali yake ya kwaida. Sura ya kawaida. Sura yake halisi. Alivua mawani. Alinyofoa yale madevu aliyoweka. Alijiangalia kwenye kioo na kuiona sura yake halisi.

Kumbuka kuwa alifanya vile ili mkewe asimtambue kule kwenye baa ya Mwenda baada ya kuambiwa huwa anakwenda na mwanaume.

Alijua kuwa akitoka, Tedi atashtuka. Hakuna na jinsi. Ni lazima arejee kwenye hali yake ya kawaida kwa sasa. Labda ikimlazimu baadaye.

Alipomaliza alitoka nje. Mshtuko mkubwa ulimpata Tedi. Alihisi anaota ndoto. Tena ndoto yenyewe mbaya ambayo hajawahi kuota tangu azaliwe. Aliyeingia kuoga, siye aliyetoka.

Alianza kukumbuka hadithi za majini ambao huwa wanajigeuza binadamu. Hata hivyo, hadithi nyingi zilieleza kuwa majini wengi waliojigeuza binadamu ni wanawake. Leo kwa mara ya kwanza anakutana na jini mwaume.

Alitaka kupiga kelele lakini haikutoka. Alijitupa kitandani macho yakiwa yamemtoka, akijua kabisa kuwa kinachofuata ni kuuawa.

Hata kama yule mtu hakuwa jini, lakini alikuwa mtu mbaya na alikuwa na nia mbaya. Alikumbuka pia hekaya wa wanyonya damu. Ambao wanawachukua wanawake, wanawatongoza na kwenda nao kwenye hoteli au nyumba za kulala wageni na kuwanyonya damu. Sasa ilikuwa ni zamu yake.

Wakati macho yakiwa yamemtoka pima, mikono alinyoosha mbele, ili kujaribu kumzuia mtu aliyetoka bafuni ambaye si yule Tom.

Tom alijua hilo. "Samahani sana Tedi. Mimi ni yule yule mpenzi wako." Tedi mpaka wakati huo alikuwa bado hajalijua jina la mpenzi wake aliyelengeshwa jana na shoga yake. Ila mwenzake alikuwa analifahamu jina lake.

Sauti ilikuwa ni ile ile. Lakini hiyo haikumfanya Tedi kuendelea kuwa na hofu. Mwili wote ulitetemeka na jasho lilimtoka.

"Samahani mpenzi. Nilijua utaogopa. Lakini sikuwa na njia yoyote ile ya kufanya. Ni lazima nirudie kwenye hali yangu ya kawaida. Niliamua kujibadilisha kwa sababu ya maswahibu yaliyonikuta. Uliniuliza nimekuja kufanya nini Morogoro. Kujibadilisha huku ndiko moja ya sababu iliyonifanya nije."




Yalikuwa ni maneno ambayo Tom aliyasema kwa ajili ya kumtoa hofu Tedi. Bado Tedi aliendelea kuwa na hofu. Mpaka wakati huo hakuongea neno lolote. Alijiona ni kama mfu anayesubiri kuuawa rasmi.

Tom aliweka mezani miwani yake pamoja na vipande vya plastiki ambavyo vilionekana kama ngozi, vikiwa pia na ndevu.

Kwa asilimia kadhaa Tedi alianza kurejewa na fahamu za kawaida. Woga ulianza kumuondoka, ingawa si kwa asilimia zote. Kilichomfanya hivyo si maneno tu. Hata vitendo vya mtu huyo mpya havikuonekana kutaka kumdhuru, wala kumtolea maneno makali. Yalikuwa ni yale yale ya mpenzi wake yule yule aliyekuwa naye kwenda baa ya Mwenda.

Alijua bado Tedi ana wasiwasi naye, hivo hakutaka kumsogelea kwa kuepusha chochote kibaya kinachoweza kutokea kutokana na woga uliokithiri.

Aliamua kukaa kwenye kiti kidogo kilicho pembeni mwa kitanda kwenye nyumba hiyo ya kulala wageni.

Alishusha pumzi. Bado Tedi alikuwa kwenye hali ya woga.

"Nakumbuka uliniuliza umekuja Morogoro kufanya nini." Alianza kuongea Tom kwa utulivu. Alijua hatojibiwa, wala kuungwa mkono kwenye mazungumzo hayo na mpenzi wake Tedi ambaye alikuwa kitandani ameegemea ukuta, mkono wake mmoja ukiwa umeshikilia kanga yale aliyojifunga na moja kuziba uso, ili asione lolote baya litakalomtokea.

"Tedi, mimi jina langu halisi ni Tom. Nimekuja Morogoro kutoka Dar es Salaam kwa ajili ya kumsaka mke wangu Farida. Yule uliomuona jana pale kwenye baada ya Mwenda ndiyo mke wangu. Yule ambaye alikuwa ameshikiliwa na jamaa mmoja aliyekuja naye. Kumbuka wakati tulikuwa tumekaa kwenye meza, ile nyingine ya pili tuliyokuwa tungaliana nayo, ndiyo aliyokuwa amekaa mke wangu na huyo jamaa."

Ingawa bado alikuwa na wasiwasi, lakini Tedi alianza kuhisi kitu.

Alianza kukumbuka kitu. Wakati wakiwa kwenye baa ya Mwenda alishuhudia jamaa mmoja akiinua na kumshika mkono, baadaye kumkumbatia mwanamke mmoja kiasi cha mpenzi wake huyo kuwaangalia kwa namna ambayo ilimkera mpaka yeye mwenyewe. Akakumbuka kuwa aliimuuliza swali na mazungumzo mafupi baada ya hapo.

"We umekolea sana na yule dada eee."

"Nini?"

"Nini nini, wewe unamwangalia sana yule dada na yule mpenzi wake, unanichefua. Sasa umeniitia nini hapa? Unawafahamu?" Akakumbuka alivyouliza.

"Hapana mpenzi, kuna mmoja kama namfananisha hivi."

**Yalikuwa ni maneno ambayo Tom aliyasema kwa ajili ya kumtoa hofu Tedi. Bado Tedi aliendelea kuwa na hofu. Mpaka wakati huo hakuongea neno lolote. Alijiona ni kama mfu anayesubiri kuuawa rasmi.**

"Nani kati ya wale?"

"Nitakwambia baadaye. Tuondoke."

"Tunakwenda wapi sasa?"

"Kwangu."

"Nyumbani kwako? Huna mke?"

"Hapana, ni kwenye hoteli nilikofikia."

"Kumbe wewe siyo wa hapa Morogoro."

"Ndiyo. Mimi natoka Dar."

Baada ya kumbukumbu hiyo, Tedi aliuachia mkono wake wa kulia usoni na kuanza kumtazama kwa chati Tom.

"Tedi, wewe ulinieleza matatizo yako, na mimi nikakuliwaza na kukubembeleza, mimi pia nina matatizo makubwa. Haya mawani, ndevu na ngozi laini hivi za bandia, nilizivaa makusudi kwa ajili ya kuficha sura yangu halisi ili mke wangu asinitambue. Ndiyo maana unaona tumekaa pale hakunitambua. Ni mimi tu ndiye niliyekuwa namtambua."

Ndipo akili ya Tedi ilipoanza kufunguka taratibu. Aliunganisha tukio lile na maneno ya mpenzi wake, akaona huenda ni kweli yanayozungumza. Woga taratibu ukaanza kuondoka.

"Alinikimbia au kunitoroka wiki moja tu baada ya kufunga ndoa. Sijafaidi kabisa raha ya ndoa. Sijajua ni kwa nini amefanya hivi. Nimekuja huku baada ya kupata taarifa za watu mbalimbali, wengine ndiyo wakaniletа hadi huku kwenye baa yenu. Wakaniambia huwa anaonekana huku akiwa na mwanaume mwingine. Ndiyo maana niliamua kujibadilisha ili nishuhudie. Na kweli nimeshuhudia, japo imeniuma sana." Alisema Tom kwa uchungu, kwa mbali machozi yalianza kumchuruzika

Woga ulikuwa umeshaondoka kabisa kwenye moyo wa Tedi, huruma ikashika nafasi yake.

Akainua kutoka kwenye kitanda. Akamsogelea taratibu mpenzi wake. Kwanza akambusu. Akamnyanyua kutoka kwenye kiti. Akamkumbatia na kumsogeza kitandani. Alichotaka kufanya ni kumliwaza na kumbembeleza, kama alivyofanyiwa yeye wakati akihadithia madhila yake.

"Pole sana baba. Pole mpenzi wangu." Tedi alimbembeleza, sasa akiwa ameshatambua kuwa Tom hakuwa jini, zimwi, wala jambazi, ila alilazimika ajibadilishe kwa ajili hiyo.

"Hapa nilipo kila kitu nimeshajua kuwa mke wangu ametorokea Morogoro na yupo na mwanaume mwingine."

"Sasa utafanyaje. Nakuomba usilipe kisasi wala kufanya jambo lolote baya."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SOLSKJAER AONYA KUHUSU SANCHO



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amekubali Jadon Sancho 'inaweza kumchukua muda' kuwa kwenye hali nzuri kiuchezaji baada ya kutua klabuni hapo akiwa amechelewa kutoka kwenye michuano ya Euro 2020.

Sancho alisajiliwa na klabu hiyo kipindi hiki cha majira ya joto kutoka Borussia Dortmund kwa ada ya pauni milioni 73 baada ya kuwaniwa na mashetani wekundu hao kwa muda mrefu, na mashabiki wanamtarajia kumuona msimu huu akikiwasha.

Lakini Solskjaer - ambaye ataiongoza timu yake katika mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu England msimu dhidi ya Leeds United leo Jumamosi - ameonya kuwa wasitarajie makubwa sana kwa nyota katika mchezo wake wa kwanza baada ya kukosa kujinoa na wenzake.

Sancho anatarajiwa kuanza kwenye mchezo huo dhidi ya kikosi hicho cha kocha, Marcelo Bielsa pale katika dimba la Old Trafford.

Na kwa mujibu wa ripoti, Solskjaer ameonya kuwa wasitarajie mchezaji huyo kuwa kwenye kiwango bora zaidi kwenye mchezo huo.

"Alikuwa likizo baada ya michuano ya Ulaya na bahati mbaya amechelewa kwenye mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya," alisema Solskjaer akiiambia televisheni ya Norway, TV2.

# Van Dijk ajifunga Liverpool hadi 2025

**LIVERPOOL.** England

MLINZI wa Liverpool, Virgil van Dijk, ameongeza mkataba wa kuitumikia klabu hiyo hadi kipindi cha majira ya joto mwaka 2025.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ambaye alikuwa na mkataba hadi mwaka 2023, amefuata nyayo za Trent Alexander-Arnold, Fabinho na Alisson kwa kusaini mkataba mpya kipindi hiki cha majira ya joto.


Alicheza mechi tano tu za Ligi Kuu England msimu uliopita, baada ya kuumia goti Oktoba, mwaka jana.

Van Dijk, ambaye amerudi uwanjani wakati wa kipindi cha maandalizi ya msimu mpya, amesema "amefurahishwa na ana furaha na anajisikia fahari," kusaini mkataba mpya.

"Kwa juhudi zote zilizofanyika hadi sasa na naangalia uwezekano wa kufanya makubwa zaidi kwa siku za mbeleni hapa Liverpool," aliongeza mlinzi huyo wa kati wa kimataifa wa Uholanzi, ambaye alicheza jumla ya mechi 130 kwa Liverpool.

"Hapa nilipo na namna ninavyojihisi, kama mchezaji mkubwa na muhimu kwa timu na klabu.

"Hizi ni hisia nzuri sana kwangu na kwa uhakika nitaendelea kujisikia vizuri hapa nyumbani."



# *Mashabiki wasusia tiketi Barcelona*

**BARCELONA,** Hispania


BARCELONA bado inaendelea kupata maumivu baada ya kuondoka kwa Lionel Messi aliyetua Paris Saint-Germain na inaonesha mashabiki hawajashawishika na lolote kuelekea kuanza kwa msimu mpya bila ya mchezaji wao huyo.

Mashabiki wameonesha kutokuwa na hamasa, kwani hadi sasa maombi ya mashabiki kununua tikeki yamefikia 15,820 kwa ajili ya mchezo wao wa kwanza wa msimu huu wa LaLiga Jumapili dhidi ya Real Sociedad.

Ni mashabiki nusu tu ndio waliotuma maombi ya kununua tiketi kwa ajili ya mchezo huu, ambapo umeruhusiwa kuwa na mashabiki 30,000.

Hayo ni maombi machache ya kununua tiketi kwa ajili ya kushudia mchezo wa kwanza kwa mashabiki kuruhusiwa uwanjani kwa kipindi cha miezi 17 kutokana na mlipuko wa virusi vya corona pale kwenye dimba la Nou Camp.

Barcelona mchezo wao wa mwisho wa ushindani kucheza mbele ya mashabiki ulikuwa dhidi ya Real Sociedad, Machi 7 mwaka 2020, wakati Messi alipofunga kwa penalti ya dakika za majeruruhi na kupata ushindi wa bao 1-0.



HABARI MICHEZO

# Man City wampandia bei Kane

**MANCHESTER.** England

MANCHESTER City ipo tayari kulipa kiasi cha euro milioni 150 kwa ajili ya kumsajili Harry Kane wakati wakijaribu kuishawishi Tottenham Hotspur kumuuza nahodha wao huyo, limedai gazeti la The Guardian kupitia mwandishi wa habari za usajili wa Italia, Fabrizio Romano.

Kane bado amebakia kuwa mchezaji wa Tottenham huku msimu mkuu wa ligi ukiwa umeshaanza jana.

Kocha wa Man City, Pep Guardiola amebainisha wazi kuwa anavutiwa zaidi na mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England.

Hadi sasa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na Spurs katika ofa hiyo ya Man City.

Spurs mara kadhaa imekuwa ikisisitiza kuwa Kane hauzwi licha ya fowadi huyo kuripotiwa kuwasilisha maombi ya kutaka kuondoka mwishoni mwa msimu uliopita.

Awali Tottenham walikataa ada ya pauni milioni 100, ambapo kiasi kama hicho City walikitumia kumsajili, Jack Grealish kutoka Aston Villa.



# NEYMAR: PSG YA MESSI HAITAFUNGIKA




**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR anafurahia kuungana na Lionel Messi pale Paris-Saint Germain na anaamini kwamba Mauricio Pochettino ni mtu sahihi kumwongoza nyota huyo.

Akiwa mchezaji huru, Messi mwenye umri wa miaka 34, alikubali kuhamia kwa miamba hao wa Ufaransa mapema wiki hii akiondoka kule Barcelona, ambako alicheza na Neymar kwa kipindi cha miaka minne na sasa wote wameungana PSG.

Dirisha la kipindi cha majira ya joto kimekuwa kitamu zaidi kwa miamba hao wa Ligue 1 kwani pia wamemtwaa nahodha wa zamani wa Real Madrid, Sergio Ramos, shujaa wa Euro 2020, Gianluigi Donnarumma na Georginio Wijnaldum pamoja na Achraf Hakimi aliyetua hapo akitokea Inter Milan kwa ada ya awali ya pauni milioni 51.3.

Na baada ya kutua kwa Messi, Neymar mwenye umri wa miaka 29, ameshindwa kuficha hisia zake namna anavyofurahia kucheza tena raia huyo wa Argentina.

Amesema: "Umekuwa usajili mkubwa kwa timu yangu. Tutakuwa timu isiyofungika," amesema Neymar akinukuliwa na vyombo vya habari vya Ufaransa.

Messi sasa atacheza pamoja na wakali wengine kama Kylian Mbappe, Angel Di Maria na Marco Veratti chini ya kocha Pochettino.

Na Mbrazil huyo akamzungumzia kocha wake na kusema: "Pochettino ni kocha mkubwa na mtu wa aina yake.

# *Alexander-Arnold alitolea jicho taji EPL*

**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold amesema malengo yake ni kubeba taji la Ligi Kuu ya England msimu huu.

Wekundu hao wa Anfield walimaliza kipindi cha kusubiri kwa miaka 30 kutwaa taji lao la kwanza la ligi hiyo, misimu miwili iliyopita.

Kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kilimaliza kikiongoza kwa tofauti ya pointi 18 dhidi ya Manchester City waliokuwa nafasi ya pili kwenye mbio za kuwania ubingwa na wakatawazwa kuwa mabingwa, zikiwa zimebakia mechi saba ligi kumalizika.

Lakini msimu uliopita walikuwa kwenye nafasi ngumu na kushindwa kutoa ushindani kwenye mbio za ubingwa huo.

Na sasa Alexander-Arnold, anaamini baada ya kupitia msimu wa kukatisha tamaa, msimu huu wana malengo makubwa ya kulinyakua taji hilo.

"Kwa sasa tunachofikiria ni kushinda tu... na mwishoni mwa Mei mwakani tuweze kulibeba taji hilo," alisema Alexander-Arnold akinukuliwa na Athletic.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LUKAKU AWEKA REKODI YA MSHAHARA CHELSEA

●●● Ndiye mchezaji anayelipwa zaidi, akimpiku N'Golo Kante ambaye alikuwa...

**LONDON,** England

ROMELU Lukaku amemzidi N'Golo Kante na kuwa mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi Chelsea baada ya kukamilisha uhamisho wa fedha nyingi kutoka Inter Milan, kwa mujibu wa The Athletic.

**Chelsea ilikamilisha usajili wa Lukaku mwenye umri wa miaka 28 kwa pauni milioni 97.5 na kuweka rekodi ya usajili wa fedha nyingi zaidi katika historia ya klabu hiyo.**

Mshambuliaji huyo alikuwa akiwindwa zaidi na kochaThomas Tuchel katika kipindi hiki cha majira ya joto kwa ajili ya kuimarisha safu yake ya ushambuliaji.

Lukaku amejiunga tena na Blues hao ambapo aliondoka na kujiunga na Everton mwaka 2013 kwa pauni milioni 28 na amesaini mkataba wa miaka mitano.

Na kwa mujibu wa ripoti hiyo, Lukaku amerudi hapo katika Klabu ya London Magharibu akiwa ndio mchezaji anayelipwa kiasi kikubwa zaidi cha mshahara kwa kikosi hicho cha Tuchel, huku mshahara wa raia huyo wa Ubelgiji ukiupiku ule wa mchezaji mwenzake, Kante anayelipwa pauni 290,000 kwa wiki.

Ripoti hiyo inasema kwamba, pamoja na haki za picha na bonasi kutamfanya Lukaku kuchukua nyumbani kiasi cha kati ya pauni 325,000 na 450, 00 kwa wiki hapo Chelsea.

Kwa mshahara huo Lukaku sasa atakuwa amempita Kante kwa pauni 160,000 kwa wiki, huku pia ukimfanya kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa kiasi kikubwa zaidi cha fedha kwenye Ligi Kuu England.

Lukaku, ambaye aliiongoza Inter Milan kutwaa taji la Ligi Kuu ya Italia, Scudetto, msimu uliopita, alionesha kuwa na furaha kubwa kuendelea kucheza huko Italia msimu huu, lakini kutokana na matatizo ya kifedha ya klabu hiyo yakailazimu kukubali ofa ya Chelsea ya pauni milioni 98.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 alikuwa hajamaliza biashara aliyoianza England, akiwa ameondoka kule Manchester United bila kuwa na mchango mkubwa kama ilivyotarajiwa.

Akizungumza mara baada ya kukamilisaha usajili wake hapo Chelsea ambapo atakuwa akivaa jezi namba 3, Lukaku alisema ana furaha kutua hapo.

"Nina furaha na kubarikiwa kurudi tena kwenye klabu hii," alisema Lukaku akinukuliwa na tovuti ya klabu hiyo.

"Ilikuwa safari ndefu kwa upande wangu, nilikuja hapa nikiwa mtoto na nilijifunza mengi, sasa nimerudi na uzoefu wa kutosha na nimepevuka."

## ZISIKUPITE

### CITY WAKOMAA NA KANE

MANCHESTER City wako tayari kulipa euro milioni 150 ili kumsajili, mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, kutoka Tottenham. ***(Guardian)***

### HARRY NA HATIMA

HARY Kane ana matumaini kuwa hatima yake itakuwa wazi zaidi wiki ijayo baada ya Tottenham Hotspur kuanza kampeni yao mpya ya Ligi Kuu England nyumbani dhidi ya Manchester City, klabu inayomtaka. ***(Telegraph)***

### PSG KUMSAJILI RONALDO 2022

KLABU ya Paris St-Germain itatafuta namna ya kumsajili mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36 kutoka Juventus msimu wa kipindi cha majira ya joto mwaka 2022 kama mbadala wa mshambuliaji wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, Kylian Mbappe, ambaye amekuwa lengo la muda mrefu la Real Madrid. ***(AS)***

### COUTINHO KURUDI LIVERPOOL

KIUNGO wa Brazil, Philippe Coutinho, mwenye umri wa miaka 29 amehusishwa na kurudi Liverpool akitokea Barcelona, klabu aliyotua kwa pauni milioni 142, Januari 2018. Everton, Manchester United, Chelsea, Arsenal, Tottenham na Leicester City hivi karibuni pia zimekuwa zikihusishwa na nyota huyo. ***(Liverpool Echo)***

### LIVERPOOL INAMTAKA DOKU

LIVERPOOL inasemekana pia inavutiwa na fowadi wa Ubelgiji, Jeremy Doku kutoka Rennes, ambayo itahitaji pauni milioni 38 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 19. ***(Voetbal24)***

### RUDIGER AWANIWA

REAL Madrid na Paris St-Germain zinafuatilia hali ya beki wa kati wa Ujerumani, Antonio Rudiger, mwenye umri wa miaka 28 kule Chelsea. ***(Sky Sport)***

### SPURS WAMTAKA TORRES

KLABU ya Tottenham Hotspur inaweza kumchukua beki wa Villarreal mwenye umri wa miaka 24, Pau Torres. ***(Express)***

### O'BRIEN AGOMBEWA

CRYSTAL Palace wamejiandaa kushindana na Leeds United katika harakati zao za kumuwania kiungo wa kati wa England na Huddersfield Town mwenye umri wa miaka 22, Lewis O'Brien. ***(Football Insider)***

### HASENHUTTL AWANIWA

KOCHA wa Southampton, Ralph Hasenhuttl ameazimia kumbakisha kiungo wa England mwenye umri wa miaka, 26 James Ward-Prowse, ambaye anawaniwa na Aston Villa na Tottenham. ***(Football London)***

### DIALLO KUONDOKA MAN UNITED

MANCHESTER United ipo tayari kumruhusu mshambuliaji wa Ivory Coast, Amad Diallo, mwenye umri wa miaka 19 kuondoka kwa mkopo msimu huu wa joto. ***(Manchester Evening News)***

# HABARI MICHEZO

## Sonso amrithi Manyama Ruvu

**Na Saada Akida**

BAADA ya kujihakikishia ataendelea kuifundisha Ruvu Shooting, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Mkwasa, amesema anatarajia kikosi chake kitaonekana tofauti na chenye ushindani katika msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana akiwa katika mapumziko mkoani Morogoro, Mkwasa alisema mazungumzo na mabosi ya klabu hiyo yameenda vizuri na wamekubaliana atabakia klabuni hapo kwa ajili ya msimu mpya utakaoanza ifikapo Septemba 29, mwaka huu.

Mkwasa alisema kwa sasa wanaendelea na mchakato wa usajili ili kukiimarisha kikosi hicho kwa kuongeza wachezaji ambao wataziba nafasi zilizoachwa wazi na nyota wake walioondoka akiwamo, Charles Manyama.

"Bado niko sana, niwahakikishia mashabiki wa Ruvu Shooting tumejipanga vizuri kwa sababu tayari tumeyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza msimu ulioisha na sasa kuna mambo mazuri yanakuja."

Aliongeza tayari wameshakamilisha mazungumzo ya kumsajili Ally Mtoi 'Sonso' kwa ajili ya kuzipa pengo liliachwa na Manyama ambaye amejiunga na Azam FC.

## Corona yakwamisha ngoma za asili

**Na Sabato Kasika**

MASHINDANO ya ngoma za asili Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, ambayo hufanyika kila mwaka wakati wa Sikukuu ya Wakulima Nanenane, yameahirishwa kutokana na tishio la ugonjwa wa corona.

Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo, ambaye ofisi yake huratibu mashindano hayo, alisema yatapangwa baada ya hali kuwa nzuri, na kuwataka wananchi kwenda kupata chanjo ya kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema, mashindano hayo ambayo hufanyika kila mwaka kwenye sikukuu ya wakulima, yalipangwa kufanyika kijijini Suguti yakishirikisha vikundi vya ngoma za asili kutoka kila kata.

"Baada ya ratiba ya mashindano kuharibika kutokana na corona, ninawahimiza wakazi wa Musoma Vijijini kwenda kupata chanjo iliozinduliwa rasmi huku kwetu tangu Agosti 9 mwaka huu," Prof. Muhongo alisema.

Alisema, huwa wanafanya mashindano hayo, ili kufufua ngoma za asili na kwaya, kuibua vipaji na kuimarisha ushirikiano miongoni mwa wakazi wa jimbo hilo, lakini safari hii wamelazimika kuahirisha kutokana na corona.

Mbunge huyo alisema, jimbo hilo lina kata 21, ambapo kila kata hutoa vikundi viwili, vinavyoshiriki katika mashindano hayo, na mwisho wa siku huwa kuna zawadi kwa washindi wa kwanza hadi wa tatu

Alizitaja baadhi ya ngoma za asili ambazo huwa zinapambanishwa katika mashindano hayo, ambayo yalianza miaka minne iliyopita kuwa ni mbegete, zeze, liranda na ritungu.

# YANGA SC YAGEUKIA USAJILI WANAWAKE

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kukamilisha karibuni asilimia 90 ya usajili kwenye timu ya wakubwa ya wanaume, klabu ya Yanga sasa imegeukia usajili kwa timu ya soka la wanawake, Yanga Princess kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Mbali na timu ya wanawake, lakini klabu hiyo itaanza usajili kwa timu ya vijana ya U20 pia.**

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, amesema kuanzia tarehe 15 wataanza usajili kwa timu ya wanawake na ya vijana kwa ajili ya kuimarisha vikosi hivyo ambavyo msimu uliomalizika, vilililetea sifa klabu hiyo.

"Kwa kiasi kikubwa tumemaliza usajili kwa ajili ya timu ya wakubwa ya wanaume, sasa kazi inahamia kwenye timu ya wanawake. Tarehe 15 mwezi huu hadi 30 ambapo ndiyo mwisho wa usajili, tutakuwa na kazi ya kusajili timu ya wanawake na timu ya vijana. Kuanzia Jumatatu tutaanza kutangaza na kuweka kwenye akaunti yetu rasmi ya mtandao wachezaji tunaowasajili na tutaowaacha. Kwa sasa klabu iko kwenye mabadiliko, kwa hiyo pia mabadiliko yapo hata kwenye utandaji. Zamani watu walikuwa wakikiona tu kikosi cha wanawake, au cha vijana kikiwa uwanjani kinacheza na kimeshasajiliwa, lakini sasa watakuwa wakihabarishwa mmoja mmoja, anayeingia kwa kusajiliwa na anayetoka, yaani kuachwa au kuuzwa au kupelekwa kwenye klabu nyingine kwa mkopo," alisema Bumbuli.

Timu ya soka ya wanawake, Yanga Princess, ilishika nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, bingwa ikiwa ni Simba Queens, huku timu ya soka ya vijana U20 ilifika fainali ya Ligi ya Vijana na kufungwa na kikosi cha pili cha Mtibwa.



Mpiga ngoma ndogo wa bendi ya Waluguru Original ya mjini Morogoro, Kelvin Sayona, akifanya vitu vyake kwenye onyesho la bendi hiyo mjini humo hivi karibuni. **PICHA: SABATO KASIKA**



# *Simba Queens yasaka makali*

**Na Saada Akida**

MABINGWA wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens wanatarajia kucheza mechi tatu za kirafiki ili kujiandaa na mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati ambayo yatafanyika kuanzia Agosti 28, mwaka huu jijini Nairobi, Kenya.

Michuano hiyo ni kwa ajili ya kupata mwakilishi wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), atakayeshiriki fainali za Afrika za Wanawake zitakazochezwa baadaye mwaka huu nchini Misri.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Hababuu Ali (pichani), alisema lengo la mechi hizo ni kukiimarisha kikosi chake kabla ya kuelekea Kenya kwenye michuano hiyo itakayoshirikisha klabu tisa kutoka nchi wanachama wa CECAFA.

Hababuu alisema mechi ya kwanza watacheza kesho dhidi ya Timu ya wasichana ya umri chini ya miaka 16 (U-16) ya JMK Park na baadaye Agosti 21 na 25, mwaka huu atajipima na timu nyingine za hapa jijini.

"Kwa timu za hapa nyumbani nimeona kikosi cha Fountain Gate, wameanza mazoezi nina imani tukipata nafasi ya kucheza nao mechi ya kirafiki huku tukiangalia timu nyingine kutoka nje itatusaidia, kazi kubwa kwa sasa ninaandaa kikosi cha kwenda kushindana," alisema Hababuu.

Simba Queens imepangwa Kundi A pamoja na Lady Doves WFC ya Uganda na PVP FC kutoka Burundi.

Michezo
Jumamosi Agosti 14, 2021
Nipashe




Lukaku aweka rekodi ya mshahara UKURASA 22



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), Patrice Motsepe (wa pili kulia), ofisini kwake jijini Dodoma, jana. Wa pili kushoto ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa. Kushoto ni Rais wa TFF, Wallace Karia, watatu kulia ni mke wa Rais wa CAF, Precious Motsepe, na wanne kulia ni Katibu Mkuu wa CAF, Veron Mosengo - Omba. **PICHA: PMO**

# Chama, Kisinda sasa timu moja

## ●●● Djuma, Moloko rasmi Jangwani, huku Kanoute akinukia Msimbazi...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

HATIMAYE klabu ya Simba imetangaza kumuuza kiungo wake mshambuliaji, Clatous Chama kwenye klabu ya RS Berkane ya nchini Morocco, huku ikiwa kwenye hatua nzuri ya kumsajili Saido Konoute kutoka nchini Mali.

**Klabu ya Berkane kwa sasa inafundishwa na kocha Florent Ibenge aliyekuwa akinoa AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).**

Kanoute anatajwa atakuwa mrithi wa Chama ambaye amesaini mkataba wa miaka mitatu na Berkane.

Kaimu Ofisa Habari wa klabu ya Simba, Ezekiel Kamwaga, amesema kuwa Chama aliyesajiliwa na Simba miaka mitatu iliyopita ameuzwa kwa makubaliano ya pande zote tatu.

"Tumemruhusu kujiunga na timu hiyo kwa sababu ofa ilikuwa ni nzuri kwa pande zote, mshahara ambao wanampa ni mara nne ya ule ambao anaolipwa Simba. Na yeye mwenyewe Chama alisema kwa sababu ameitumikia klabu hii kwa uaminifu na mapenzi makubwa, basi aliomba tu aende akafatute changamoto kwingine pamoja na maslahi zaidi," alisema Kamwaga.

Hata hivyo, hakutaka kusema kiasi cha bei ambayo Simba imemuuza kiungo hiyo, lakini habari za ndani zinasema inakadirishwa kiasi cha Sh. bilioni 1.5 kwa fedha za Kitanzania.

Chama ambaye alisajiliwa Simba Julai 2018, sasa anajiunga na aliyekuwa winga wa Yanga, Tuisila Kisinda ambaye naye alipigwa bei na klabu hiyo, ambao wamekutana timu moja.

Taarifa zaidi zilizolifikia gazeti hili kwamba, uongozi tayari uko kwenye hatua za mwisho za kuinasa saini ya Konoute anayekuja kuimarisha kikosi cha Wekundu wa Msimbazi hao.

Mtoa habari wetu kutoka ndani ya klabu hiyo, ameliambia gazeti hili kuwa kamati ya usajili imekuwa makini katika suala la usajili hasa kuziba nafasi ya wachezaji wanaondoka ikiwamo Chama ambaye nafasi yake itachukuliwa Kanoute.

Alisema Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, imedhamiria kufanya usajili mzuri kwa kuimarisha kikosi cha timu hiyo kulingana na mapendekezo ya kocha mkuu, Didier Gomes.

Simba tayari imewasajili nyota watano wazawa ambao ni kipa Jerimiah Kisubi (Tanzania Prisons), Abdulswamad Kassim, Yusuph Mhilu (Kagera Sugar), Denis Kibu (Mbeya) na Israel Mwenda kutoka KMC FC na mchezaji mmoja wa kigeni, Peter Banda.

**Wakati huo huo**, Klabu ya Yanga imewatambulisha rasmi wachezaji wawili kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Djuma Shaaban na Jesu Moloko kuwa ni mali yao na wataanza kuitumkia kuanzia msimu ujao wa Ligi Kuu 2021/22.

Wachezaji wao ambao wote wametokea AS Vita Club, wametambulishwa kwenye mtandao rasmi wa kijamii wa klabu hiyo jana majira ya saa 9:00 Alasiri, baada ya tetesi za muda mrefu za wachezaji hao kutua Jangwani. Mpaka sasa Yanga imeshawasajili wachezaji Fiston Mayele, Heritier Makambo, Djigui Diarra, Yusuph Athumani, Erick Johora, na Dickson Ambundo.

# Majaliwa ateta na Rais CAF kukuza soka nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, jana alikutana na Rais wa Shirikisho la Mpira barani Afrika (CAF), Dk. Patrice Motsepe na kujadiliana naye masuala muhimu ya kuendeleza michezo nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu wakati wakizungumza ofisini kwake Mlimwa, jijini Dodoma, Majaliwa alimweleza mikakati ambayo serikali inatumia ili kuinua kiwango cha soka nchini.

"Sisi tumeanza kuboresha michezo nchini chini ya mpango unaohusisha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

"Mpango huu unalenga kuibua vipaji vya vijana kupitia mashindano ya UMITASHUMTA, UMISETA, Vyuo Vikuu na Vyuo vya Kati," alisema Majaliwa.

Katika mazungumzo yao, walijadiliana suala la kuendelea kutenga bajeti ya kuinua michezo kwa vile nchi nyingi zinashindwa kufanya vizuri kwenye michezo kwa sababu hazitengi bajeti.

"Nimemweleza kuwa hapa kwetu kupitia Bunge letu tukufu, tumekuwa tukitenga bajeti hiyo japokuwa tunajua kuwa haitoshelezi mahitaji yote."

"Kuhusu uendelezaji wa michezo nchini, Rais wa CAF ametusihi tuwe na mpango madhubuti wa kupata maeneo ya kufanyia mazoezi, tuwe na viwanja bora vyenye vipimo vya kisasa, jambo ambalo nimemweleza linatekelezwa na shirikisho la soka nchini.

"Pili, ametutaka tuandae vijana kuanzia umri mdogo, tuwe na taasisi za serikali na za sekta binafsi zinazofundisha soka, waamuzi, makocha ili tuwaibue akina Samatta wengi zaidi kwani na sisi tunaamini kuwa wapo."

Kwa upande wake, Motsepe amesema katika uongozi wake amelenga mambo makuu matatu ambayo ni haja ya sekta binafsi kuwekeza kwenye michezo na kuongeza udhamini; ujenzi wa vituo vya michezo na vituo vya kuendeleza vijana.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >